# Nipashe

Alhamisi Machi 26, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580189

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Baraza la Madiwani laitishwa kukiwa na katazo mkusanyiko

UKURASA 2




UKURASA 13

**TISHIO CORONA**

# Wanafunzi shule binafsi sasa wasoma kimtandao

**WAZIRI** wa Afya aahidi kutoa taarifa leo, serikali yaagiza kasi iongezwe uzalishaji vitakasa mikono...

*Endelea ukurasa 2*



## BAA LA CORONA

MAAMBUKIZO ya virusi vya corona yameendelea kushika kasi duniani, yakibisha hodi katika familia ya kifalme Uingereza baada ya Mwanamfalme Charles kubainika kuwa na virusi hivyo jana. Chukua tahadhari!

* Epuka mikusanyiko ya watu
* Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
* Epuka kusalimiana na kushika mikono na kukumbatiana
* Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo




Mafundi wa kampuni ya Hipway Botek, wakiendelea na kazi ya ujenzi wa awamu ya pili ya mradi wa barabara ya mabasi yaendayo haraka kutoka Mbagala hadi Gerezani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## MWALIMU ADAIWA KUBAKA M'FUNZI

UKURASA 3

# Mwenyekiti CCM kortini tuhuma kughushi uteuzi

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** **TSHISHIMBI AIITA SIMBA MEZANI** UK. 32

**MAONI, KATUNI UK.6**

HABARI KITAIFA

## Baraza la Madiwani laitishwa kukiwa na katazo mkusanyiko

**Na Mwandishi Wetu**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Iringa, imeitisha mkutano wa Baraza Maalum la Madiwani licha ya kuwapo kwa katazo la mikusanyiko lililotolewa na serikali kukabiliana na maambukizo ya ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona.

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba IMC/C.40/23/VO II/188 ya Machi 25 mwaka huu kwenda kwa Mstahiki Meya na wajumbe wa baraza hilo iliyotiwa saini na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Hamis Njovu, wajumbe wote wanatakiwa kuhudhuria mkutano huo.

"Napenda kuwataarifu kuwa mkutano wa Baraza la Madiwani utafanyika Machi 26 mwaka huu, siku ya Alhamisi (leo) kuanzia saa 2:00 asubuhi katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri.

"Kwa barua hii, mnaalikwa rasmi kuhudhuria mkutano huo bila kukosa, menejimenti inaomba radhi kwa usumbufu ambao umejitokeza," ilisomeka sehemu ya barua hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu kuitishwa kwa mkutano huo, Mbunge wa Iringa Mjini, Mchungaji Peter Msigwa, alidai anachojua kikao hicho kimeitishwa kwa ajili ya kumng'oa Meya wa Manispaa hiyo.

"Tunachoshangaa kuna tishio la corona na ndiyo sababu iliyotumika kuahirisha kikao cha Baraza la Madiwani jijini Mbeya, hapa kesi ya kupinga kuvuliwa umeya inatolewa uamuzi Machi 27 mwaka huu (kesho) kwamba mchakato wa kumvua uendelee au usiendelee na siku moja kabla, wameitisha kikao cha madiwani na wanataka kumvua umeya.

"Tunashangaa wanataka kufanya kikao hiki, tunachoona serikali haiko 'serious' (makini) na corona, tumekubaliana kusiwe na mikusanyiko, lakini wao wanaitisha mkutano ambao ni mkusanyiko," alisema.

Mbunge huyo alisema analazimika kuhudhuria mkutano huo licha ya kuwapo kwa tishio la maambukizo ya corona kwa kuwa asipohudhuria, ataathiri akidi ya chama chake cha Chadema.

Machi 17 mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza uamuzi wa serikali wa kufunga shule za awali, msingi na sekondari na kuzuia mikusanyiko ya mikutano, semina, warsha, makongamano na mikusanyiko mingine ili kujilinda dhidi ya uwezekano wa kusambaa kwa corona.



Naibu Balozi wa Saudi Arabia nchini, Abdulaziz Hamad Alasim, akikabidhi sehemu ya kompyuta 120 na mashine za kudurufu saba kwa Mbunge wa Viti Maalum mkoa Dodoma, Fatma Toufiq, jijini Dar es Salaam jana, vilivyotolewa msaada na taasisi ya King Salman Humanitarian Aid and Relief Centre kwa ajili ya kusaidia shule za msingi, sekondari na ofisi za wilaya za UWT, mkoani Dodoma. **PICHA: JOHN BADI**

# Wanafunzi shule binafsi waendelea kimtandao

**Na Mary Geofrey**

WAKATI shule zote nchini zimefungwa kwa siku 30 kuanzia Machi 17 mwaka huu kutokana na tishio la virusi vya corona, baadhi ya shule binafsi zimeendelea kufundisha wanafunzi wakiwa nyumbani.

Shule hizo zinaendelea na utoaji elimu kwa mtandao kwa kuwatumia wazazi kazi za kufanywa na wanafunzi na baadaye kupewa mrejesho na hata kupatiwa kazi iliyofanywa na mwanafunzi husika ili kupitiwa na walimu.

Wazazi waliozungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam kuhusu utaratibu huo, walipongeza uamuzi huo wa baadhi ya shule nchini kwa kuwa unasaidia wanafunzi kuzingatia masomo wakati wakiwa nyumbani.

Baadhi ya wazazi hao pia walisema kuna kazi ambazo huwa wanazifuata shuleni za kila wiki na wapo wanaowasiliana na walimu wa madarasa husika na kutumiwa kazi hizo kwa njia ya mtandao zikiwa na majibu yake, hivyo mzazi kupewa jukumu la kusahihisha.

"Napongeza utaratibu huu, nilipigiwa simu niende nikachukue kazi za mwanafunzi kesho (leo), nimefurahi sana kwa sababu mtoto kukaa nyumbani siku 30 bila kufanya kazi yoyote kutamfanya abobee kwenye michezo na kusahau masomo ya darasani," alisema mmoja wa wazazi hao.

Alisema ni ubunifu mzuri kwa sababu mzazi atatoa kazi za watoto na kuzisahihisha, hivyo kutawafanya wanafunzi kuendelea kujifunza.

Mzazi wa watoto wawili, Jenifer John ambaye ni mkazi wa Sinza jijini, alisema shule kutoa kazi kwa wanafunzi waliolazimika kukaa nyumbani kwa siku 30 kunawasaidia watoto kujielekeza kwenye masomo badala ya kuzurura na kucheza mitaani. Alitoa wito kwa wazazi kuhakikisha wanasimamia watoto wao ili wafanye kazi walizopewa na walimu ili kuwasaidia katika kipindi cha mwezi mmoja walichofunga.

"Siku ya Jumatatu nilipokea ujumbe ukinitaka niende shuleni kwa ajili kuchukua kazi za watoto ambazo wanatakiwa kuzifanya ndani ya wiki moja na kutakiwa kuzirejesha ili zisahihishwe na kupewa nyingine," alisema.

Nipashe pia imebaini baadhi ya shule za serikali, hasa za vipaji maalum, nazo zinatoa kazi kwa wanafunzi. Shule hizo zimewapa wanafunzi vitabu na kuwataka kujisomea wakiwa nyumbani.

Mzazi wa mwanafunzi katika moja ya shule hizo za serikali jijini Dar es Salaam, alisema wanafunzi walipewa vitabu na kutakiwa kuvisoma katika kipindi chote cha mwezi mmoja wa kukaa nyumbani.

"Kama wazazi tumehimizwa na walimu kuwasimamia wanafunzi kusoma vitabu walivyonavyo na kuwasaidia masomo ambayo yanawashinda ili kuwafanya waendelee kusoma wakati wote wa likizo, ni jambo jema," alisifu.

Machi 17 mwaka huu, serikali kupitia kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ilitangaza kuzifunga shule zote kuanzia awali hadi kidato cha sita, na siku moja baadaye ikafunga vyuo vikuu na vya kati ikiwa ni hatua mojawapo za kukabiliana na maambukizo ya virusi vya corona.

**WIZARA KUTOA TAARIFA LEO**

Jana, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliahidi kutoa taarifa leo kuhusu hali ya ugonjwa huo nchini.

# Waziri Bashungwa aagiza uzalishaji zaidi vitakasa mikono

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, jana amekutana na wazalishaji wa vitakasa mikono (sanitizer) ili kuweka mikakati ya pamoja na kuongeza uzalishaji kutokana na tishio la ugonjwa wa corona.

Akifungua kikao hicho, Bashungwa alisema chimbuko la kikao hicho ni kutokana na ziara aliyoifanya kwenye maduka na viwanda vinavyotengeneza bidhaa hiyo na kubaini kuwapo uhaba wa vitakasa hivyo.

Alisema kikao hicho kitatoka na mikakati ya kupambana na ugonjwa huo kwa kuhakikisha vitakasa hivyo vinazalishwa kwa wingi na kukidhi mahitaji.

"Ili kupambana na ugonjwa wa corona ni kuzingatia kanuni za usafi, chimbuko la kikao ni ziara niliyoifanya Dar es Salaam kuangalia bei na upatikanaji wa vitakasa mkono lakini tulienda hadi viwandani, tuligundua kuna changamoto kwenye maduka na mikoa," alisema.

Alisema pia katika ziara hiyo walibaini kuuzwa kwa bei kubwa na kulazimika kuitisha kikao hicho kujua kero wanazokabiliana nazo na uhitaji wa malighafi.

"Kupambana na corona kunahitaji ushirikiano wa pamoja na serikali, hivyo tuangalie serikali itimize majukumu yapi na wazalishaji mtimize wajibu gani," alisema.

Alisema lengo ni kuhakikisha uzalishaji unaongezwa na kupatikana kwenye maeneo yote nchini na kwa wingi kutaondoa kero ya bei. "Nilishaagiza Tume ya Ushindani (FCC) na Shirika la Viwango nchini (TBS), kufanya msako nchi nzima ili kuwachukulia hatua wanaotaka kujitajirisha kwa mgongo wa Watanzania," alisema.

Bashungwa alisema linatakiwa kuwapo soko huria la kuangalia utu na si kuwakomoa watu.

"Mwongeze uzalishaji wa vitakasa mikono na hata sabuni, upatikanaji wa ethanol, pale Tirdo wameanza tumewaambia wazalishe kwa wingi maana kuna kiwanda tulienda wakasema wanalazimika kuagiza ethanol nje ya nchi," alisema.

Kadhalika alisema, kama wakizalisha kwa wingi wanaweza kuuza nje ya nchi.

# Mwenyekiti CCM Dodoma kizimbani tuhuma rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Dodoma Mjini, Robert Mwinje (39), amefikishwa katika Mahakama ya Mkoa wa Dodoma, akikabiliwa na mashtaka ya kula njama, kughushi na kuwasilisha nyaraka za uongo za uteuzi wa waombaji wa uongozi ndani ya chama hicho.

Mwinje aliondolewa katika nafasi yake Desemba 18 mwaka jana kutokana na kile kilichoelezwa na chama kuwa ni matumizi mabaya ya madaraka.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wamemfikisha Mwinje na Nyemo Malenda (20) kwa makosa hayo.

Kamanda Kibwengo alisema Mwinje na mwenzake wanadaiwa kutenda makosa hayo kinyume cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 na marejeo ya mwaka 2018. "Uchunguzi wetu umeonyesha kwamba kati ya tarehe 18 na 20 Oktoba 2019, Mwinje na Malenda ambaye ni Mhudumu wa Ofisi, walighushi barua ya uteuzi ya waomba uongozi ndani ya chama na huku wakijifanya imetolewa na uongozi wa CCM Wilaya ya Dodoma Mjini, wakaikabidhi kwa mwanachama mmoja kwa hatua huku wakifahamu kwamba ni uongo," alisema.

Katika hatua nyingine, Takukuru imempandisha kizimbani Mwalimu Mkuu wa Shule Msingi Msisi ya Wilayani Dodoma, David Mdeka (44), kwa tuhuma za matumizi mabaya ya nyaraka na kumdanganya mwajiri kwa kughushi muhtasari wa kikao na kutoa benki Sh. milioni moja.

Alisema mwalimu anadaiwa kutoa fedha hizo benki na kuzifuja kwa maelezo ya kununua vifaa ambavyo havikufikishwa shuleni na ukarabati haukufanyika.

Pia, Kibwengo alisema wanatarajia kumfikisha mahakamani Ofisa Mtendaji wa Kata ya Thawi wilayani Kondoa, Hashimu Ally (42), kwa madai ya kuomba rushwa ya Sh. 155,000, akidai kuwa tayari alishapokea Sh. 60,000 kutoka kwa mwananchi ili asimchukulie hatua kwa kosa la mjukuu wake kutohudhuria shuleni kwa siku 31.

Alidai kuwa baada ya kufanyika uchunguzi, ilionyesha mwanafunzi huyo alifuata taratibu za uhamisho na kufanikiwa kwenda shule nyingine.

Pia, Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Bahi, Adam Richard (49), amefikishwa mahakamani na kufunguliwa mashtaka manne ya kuomba rushwa ya jumla ya Sh. milioni 3.5 huku akidaiwa kupokea Sh. 1,050,000 kutoka kwa walimu wanne ili awasaidie katika mchakato wa kupandishwa madaraja. Aliwataka watumishi wa umma kuzingatia kanuni, sheria na taratibu za utumishi na kujiepusha na vitendo vya rushwa.

## Mwalimu mbaroni tuhuma kubaka mwanafunzi wake

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MWALIMU wa Shule ya Sekondari Milundikwa, Kata ya Nkandasi wilayani Nkasi mkoani Rukwa, anashikiliwa na polisi mkoani humo kwa tuhuma za kumbaka mwanafunzi wa kidato cha pili (17) katika shule hiyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Justine Masejo, alidai jana kuwa tukio hilo lilitokea Machi 15 mwaka huu majira ya usiku, mwalimu huyo (37), akidaiwa kumbaka mwanafunzi wake katika nyumba ya kupanga ambayo mwanafunzi huyo alikuwa anaishi.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji iliko shule hiyo, Benazir Kalamba, alidai ofisi yake ilipata taarifa kuwa mwanafunzi huyo amebakwa na mwalimu wake usiku majira ya saa sita, na baada ya kuzipata, naye akatoa taarifa kwa Ofisa Elimu wa Wilaya ya Nkasi ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Alidai Ofisa Elimu alitoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ndipo mwalimu huyo akakamatwa na mpaka sasa anashikiliwa na jeshi hilo wakati upelelezi ukiendelea.

Makamu Mkuu wa Shule hiyo, Charles Mwamengo, alisema tukio hilo limejitokeza ikiwa ni siku chache baada ya uongozi wa shule hiyo kuketi kikao na walimu na kuwaonya kuhusu tabia ya kujihusisha kimapenzi na wanafunzi.

Alisema kwa muda mrefu kumekuwa na taarifa kuwa baadhi ya walimu wa shule hiyo wamekuwa na tabia ya kujihusisha na mapenzi na wanafunzi wao.


TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

**HUDUMA ZA TRA KWA NJIA YA MTANDAO**

Ndugu mlipakodi TRA inakukumbusha kuwa, huduma zifuatazo zinapatikana kwa njia ya mtandao bila kulazimika kufika ofisini;-

1. Usajili wa TIN unaotumia namba ya kitambulisho cha taifa,
2. Makadirio na malipo ya kodi ya majengo,
3. Kujisajili kwa ajili ya kufanya malipo ya kodi moja kwa moja kupitia mfumo wa Revenue Gateway System na GePG,
4. Kuwasilisha kadhia za forodha kupitia mfumo wa TANCIS,
5. Kikokotoo cha magari yaliyotumika na kununuliwa kutoka nje ya nchi,
6. Kikokotoo cha kodi za ajira,
7. Minada kwa njia ya mtandao,
8. Maulizo na uwasilishaji malalamiko katika kituo cha huduma,
9. Kuchapisha cheti cha kodi ya zuio,
10. Uwasilishaji wa ritani za kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

Kumbuka kuwa, unaweza kupata fomu mbalimbali kwa kutembelea tovuti yetu ya www.tra.go.tz

Kwa mawasiliano zaidi tufikie kwa kutumia mawasiliano yafuatayo;-

Simu za bure: 0800-750075 au 0800-780078

WhatsApp: 0744-233 333

Barua pepe: huduma@tra.go.tz

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

156808

TANGAZO

# TPB BANK PLC

Tpb Bank Grow with us

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA [MAHESABU YALIYO KAGULIWA]

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha [Uoneshaji] ya Mwaka 2014**

### TPB BANK PLC
### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA, 2019
*Kiasi kwa shilingi milioni*

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-19 | Mwaka uliopita 31-Dec-18 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 37 749 | 23 718 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 25 827 | 13 196 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 100 588 | 56 819 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 7 946 | 15 821 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 4 | 221 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 6 611 | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 420 594 | 412 769 |
| 12 | Mali Nyingine | 16 789 | 22 245 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 21 891 | 17 556 |
| | Haki ya matumizi ya mali | 9 186 | - |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **647 184** | **562 345** |
| B | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 442 177 | 390 606 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 1 096 | 1 527 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 4 126 | 7 970 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 2 054 | 3 380 |
| 27 | Dhima Nyingine | 15 952 | 13 011 |
| | Dhima ya kukodisha | 7 314 | - |
| 28 | Madeni | 75 572 | 62 931 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **548 291** | **479 424** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **98 893** | **82 920** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 28 072 | 28 072 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | 3 913 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 44 710 | 28 437 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 15 891 | 12 102 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 10 220 | 10 397 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **98 893** | **82 920** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo Chechefu | 25 132 | 34 473 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 19 306 | 17 806 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 70 | 30 |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 15.28% | 14.75% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.67% | 7.92% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 85.61% | 95.84% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 64.99% | 73.40% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 81.55% | 88.83% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 13.20% | 18.55% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 15.09% | 22.63% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
### KWA MWAKA UNAOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2019
*Kiasi kwa shilingi milioni*

| | Limbikizo la Mwaka Wa Sasa 31-Dec-19 | Limbikizo la Mwaka Linganishi [Mwaka Uliopita] 31-Dec-18 |
|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 100 177 | 95 945 |
| 2 Gharama za Riba | (22 496) | (17 870) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **77 681** | **78 075** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | (1 265) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (10 533) | (13 656) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **29 539** | **22 371** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 2 074 | 3 492 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 20 851 | 14 867 |
| 6.3 Gawio | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 6 614 | 4 012 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(73 680)** | **(68 337)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 35 719 | 31 280 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 526 | 5 493 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 37 436 | 31 563 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **23 006** | **17 188** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 7 115 | 5 086 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **15 891** | **12 102** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | **133** | **619** |
| 11.1 Hasara ya sasa kutoka kwa wajibu wa faida | 190 | 884 |
| 11.2 Kodi kadirio la mbeleni la mafao ya mtumishi | (57) | (265) |
| 11.3 Gharama ya zamani juu ya wajibu wa faida | - | - |
| 11.4 Kodi iliyopungua kwa gharama ya zamani kwenye wajibu unaofafanuliwa | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **16 024** | **12 721** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 926 | 888 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 571 | 431 |
| 15 **Idadi ya Matawi** | 38 | 36 |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.65% | 2.26% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 17.63% | 15.34% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 56.80% | 57.76% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 12.84% | 16.08% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

### TPB BANK PLC
### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
### KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA, 2019
*Kiasi kwa shilingi milioni*

| | | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-19 | Limbikizo la Mwaka Linganishi [Mwaka Uliopita] 31-Dec-18 |
|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 23 006 | 17 188 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | - Hasara Katika Mali | 13 756 | 7 144 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (9 325) | (90 108) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 2 | (149) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 51 578 | 67 572 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (32 321) | (5 142) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (4 417) | 9 046 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 3 271 | (889) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (6 900) | (6 084) |
| | - Kodi kadirio la mbeleni la mafao ya mtumishi | (490) | 1 951 |
| | - Gharama ya mafao ya mtumishi | 1 091 | (420) |
| | - Mengineyo (Mapato ya ruzuku & hifadhi nyingine) kutoka muunganiko wa biashara ) | (42) | 4 794 |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | ***39 210*** | ***4 905*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (4 001) | (6 341) |
| | Ununuzi wa Mali Zisizoonekana | (1 409) | (2 353) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 1 | 154 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | ***(5 410)*** | ***(8 539)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (1 210) | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 888 | 526 |
| | Malipo ya Dhima ya Kukodisha | (4 992) | - |
| | Mengineyo (Kodi katika Hisa za Ziada) | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | ***(5 314)*** | ***526*** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **28 487** | **(3 108)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 5 260 | 8 368 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **33 746** | **5 260** |

### TPB BANK PLC
### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2019
*Kiasi kwa shilingi milioni*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo [bainisha] | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28 072** | **-** | **40 539** | **135** | **3 913** | **10 262** | **82 920** |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | 4 048 | (135) | (3 913) | - | **-** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya | - | - | 15 891 | - | - | - | **15 891** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Hisa za ziada | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | (1 210) | - | - | - | **(1 210)** |
| Hasara ya sasa ya manufaa yalifafanuliwa baada | - | - | 133 | - | - | - | **133** |
| Kurudishwa kwa Gawio lililosimamishwa | - | - | 1 200 | - | - | - | **1 200** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | (42) | **(42)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28 072** | **-** | **60 601** | **(0)** | **0** | **10 220** | **98 893** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28 072** | **-** | **28 386** | **288** | **3 101** | **-** | **59 846** |
| **Mabadiliko ya IFRS 9** | - | **-** | 1 291 | - | - | **-** | **1 291** |
| Hamisho kwenda hifadhi ya udhibiti | - | **-** | (1 291) | 1 291 | - | **-** | **-** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya | - | **-** | 12 102 | - | - | **-** | **12 102** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | **-** | - | - | - | **-** | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | **-** | - | - | - | **-** | **-** |
| Hisa za ziada | - | **-** | - | - | - | **-** | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | **-** | - | - | - | **-** | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | **-** | - | - | - | **-** | **-** |
| **Gawio lililolipwa** | - | **-** | (1 200) | - | - | - | **(1 200)** |
| faida ya sasa ya manufaa yalifafanuliwa | - | **-** | 619 | - | - | - | **619** |
| Hamisho kutoka/kwenda hifadhi ya udhibiti | - | **-** | 632 | (1 444) | 812 | - | **-** |
| Mengineyo | - | **-** | - | - | - | 10 262 | **5 220** |
| Salio la mwisho wa mwaka | **28 072** | **-** | **40 539** | **135** | **3 913** | **10 262** | **82 920** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA, 2019**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| **MR.S.K.MOSHINGI**<br>Ofisa Mtendaji Mkuu | | **05.03.2020** |
| **MS. REGINA E. SEMAKAFU**<br>Mkuu wa Fedha | | **05.03.2020** |
| **MR. S.NYENYEMBE**<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | | **05.03.2020** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| **DR. EDMUND B. MNDOLWA**<br>Mwenyekiti wa Bodi | | **05.03.2020** |
| **MR. MACRICE D. MBODO**<br>Mjumbe wa Bodi | | **05.03.2020** |

215681402

Head Office: LAPF Towers Bagamoyo Roard. P.O. Box 9300 Dar es Salaam Tanzania. Telephone: +255 22 2162940, Fax: +255 22 2114815, Email: info@tpbbank.co.tz

TANGAZO

Tpb Bank
Grow with us

# TPB BANK MINIMUM DISCLOSURE OF BANK RATES AND CHARGES

| TYPE OF CHARGE | TRANSACTION / ITEM | CHARGES |
|---|---|---|
| Minimum Opening Balance | Quick Account | 20,000 |
| | Salary Account | FREE |
| | Platinum Account | 15,000 |
| | Call Account | 100,000 |
| | Minor Account | 20,000 |
| | Scout Minor | 10,000 |
| | Scout | 30,000 |
| | WADU | 20,000 |
| | YANGA VIP Card | 1,200,000 |
| | YANGA Member Card | 25,000 |
| | Group Account | FREE |
| Bank Statement | | Within a month is FREE and more than a month is 1,500 per document |
| Monthly Maintenance Fee | Savings Account | 1,300 |
| | Current Account | 6,500 |
| | Platinum Account | 1,300 |
| | WADU Account | FREE |
| | Call Account | 6,500 |
| | Minor Account | FREE |
| | Group Account | FREE |
| Dormant Accounts Fee | 1 year to 5 years | 1,300 |
| | 6 years to 10 years | 5,000 |
| | 11 years to 15 years | 10,000 |
| | | |
| Activation of Dormant Account | | FREE |
| ATM Charges | ATM Balance Enquiry- All cards | 300 |
| | Mini statement | 300 |
| | Cash Withdraw on TPB ATMs | 1,300 |
| | Cash Withdraw on other UMOJA SWITCH ATM | 1,300 |
| POS Branches | Balance Enquiry | 150 |
| | Mini statement | 150 |
| | Deposit | FREE |
| | Transfer | 650 |
| | POS Withdraw | 2,600 |
| POS Agents | Balance Enquiry | 150 |
| | Mini statement | 150 |
| | Deposit | FREE |
| | Transfer | 650 |
| | POS Withdraw | see Tiered Fees 1 |
| Mobile Banking | Balance Enquiry | 300 |
| | Mini statement | 300 |
| | Full Statement | 400 |
| | Pin Charge | FREE |
| | Notification /Alert | 200 |
| | Account Transfer | 650 |
| | Mobile Agent Deposit | 200 |
| | Mobile Agent Withdraw | see Tiered Fees 2 |
| | Mobile Money to Bank Deposit | 1,300 |
| Closing Account | | 13,000 |
| FDR Min. Opening Balance | | 100,000 |
| ATM Issuance and Replacement Fees | Popote Card | 15,000 |
| | Yanga Member card | 20,000 |

| TYPE OF CHARGE | TRANSACTION / ITEM | CHARGES |
|---|---|---|
| Other ATM & Normal Card | Pin Re-issue | FREE |
| | Collection of ATM crad at Non Domicile Branch | 6,500 |
| | Uncollected and destroyed ATM card | 6,500 |
| | First ID card (Local and Foreign Currency) | 4,000 |
| | Replacement Of ID card | 2,600 |
| Cash withdraw | Teller withdraw upto 10,000,000 | 2,600 |
| | Teller withdraw from 10,000,001 to 50,000,000 | 5,000 |
| | Teller withdraw from 50,000,0001 to 100,000,00 | 15,000 |
| | Teller withdraw above 100,000,001 | 30,000 |
| Cheques Fees | Cheques Clearing Fee | 3,000 |
| | Special Clearance | 50,000 |
| | Dishonoured Cheque | 35,000 |
| Electronic Fund Transfer (EFT) | TISS Inwards | FREE |
| | TISS- Outward | 10,000 |
| Standing Order | Within the Bank | 1,300 |
| | To other Banks | 13,000 |
| POS Withdraw &Money Transfer/ Tiered fees | POS Withdraw | Tiered 1 |
| Tiered 1 | 0-10,000 | 800 |
| | 10,001-50,000 | 1,000 |
| | 50,001-100,000 | 1,300 |
| | 100,001-250,000 | 2600 |
| | 250,001-500,000 | 4,600 |
| | | |
| Tiered 2 | TPB Mobile Transfer Fee | Tiered 2 |
| | 0-10,000 | 850 |
| | 10,001-50,000 | 1,200 |
| | 50,001-100,000 | 1,500 |
| | 100,001-250,000 | 2,800 |
| | 250,001-500,000 | 4,600 |

## RATES AND CHARGES FOR USD ACCOUNT

| | | |
|---|---|---|
| Maintenance Fee | Savings Account | 1 |
| | Current Account | 5 |
| | | |
| Deposit Fee | Non Account Holder | Free |
| | | |
| Opening Balance | | 50 |
| | | |
| Account closure fee | | 10 |
| Bank Statements | | Free |
| | Balance Enquiry- Banking Hall | Free |
| | Confirmation letter | Free |
| | | |
| Withdraw Fees | 0-5,000 | 5 |
| | Above 5,000 | 20 |
| Cheque | Special clearance | 40 |
| | Unpaid cheque- Refer to Drawer | 10 |
| | Stop Payment | 20 |
| Dormant | Dormant Account Fee | 5 |
| | Re- Activation | Free |
| | | |
| TISS | | 10 |

215681402

Tpb Bank
Grow with us

+255 787 669 977 tpbbank//facebook tpbbank//instagram www.tpbbank.co.tz

## LENDING INTEREST RATES AND OTHER CHARGES

### 1. FEES ON CONSUMER LOANS

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 1. | Consumer Loan Administration Fee | 1.5% of the Approved Loan. Minimum TZS. 10,000/= |

### 2. FEES ON WASTAAFU LOANS

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 2. | Loan Application Fee | TZS. 10,000/= |
| 3. | Loan Administration Fee | 1.5% Minimum. TZS. 10,000/= Maximum TZS. 100,000/= |

### 3. OTHER CHARGES ON INDIVIDUAL MICRO CREDIT

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 1. | MIC Loan Application Fee | TZS. 20,000/= |
| 2. | MIC Loan Processing/Administration Fee | 1.5% Minimum TZS. 50,000/= |

### 4. INTEREST RATES AND OTHER CHARGES ON BUSINESS LOANS

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 1. | Loan Application Fees for Business and Personal Loans | TZS. 50,000/= |
| 2. | Loan Administration Fee - Business and Personal loans | 1.5% of the Approved Amount |
| | | |



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari corona iwekwe kwenye masoko, magulio

**WAKATI** hatua mbalimbali za tahadhari zikiendelea kuchukuliwa nchini kwa lengo la kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona, kuna kasoro ambazo tumezibaini, hivyo hatua zinapaswa kuchukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi.

Ufuatiliaji wetu katika maeneo kadhaa ya biashara yenye idadi kubwa ya watu kwa mfano katika Soko Kuu la Kariakoo, jijini Dar es Salaam tumebaini kuwa hakujawa na hadhari ya kutosha kuepukana na uwezekano wa watu kuambukizwa.

Katika maeneo hayo watu wengi wanaonekana aidha kupuuza au kutokuwa na uelewa wa maelekezo yaliyotolewa na serikali kuhusiana na hatua za kuchukua kama tahadhari ya kujiepusha na maambukizi.

Licha ya serikali kuwaagiza wafanyabiashara kuweka maji na vitakasa mikono kwenye maeneo ya biashara zao, lakini baadhi ya wafanyabiashara eneo la Kariakoo wameonekana kupuuza agizo hilo ambalo lina lengo la kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo tishio duniani ambao umeshaua maelfu ya watu katika nchi kadhaa.

Baadhi ya maduka sokoni humo yanayotembelewa na mamia ya watu yalishuhudiwa bila kuwa na ndoo zenye majisafi yenye mabomba ya kuyatiririsha, sabuni za maji na vitakasa mikono.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wafanyabiashara hao walisema hawajaweka vifaa hivyo kwa sababu vinauzwa ghali.

Mfanyabiashara wa vyombo vya nyumbani, alisema kuwa hawajaweka vifaa hivyo kwa sababu hawajaelimishwa.

Alisema Jumamosi na Jumapili ameambiwa na wenzangu kuwa magari ya manispaa yalipita kutoa elimu ya matumizi ya vitakasa mikono au sabuni za maji na maji yanayotiririka.

Alisema baada ya wenzake kumwelimisha, wapo kwenye harakati ya kutafuta fedha ili kununua vifaa hivyo kwa ajili ya kujikinga na pamoja na wateja wao.

Mwingine anayeuza urembo, sokoni hapo, alisema elimu ya corona ameipata, lakini changamoto inayowakabili wafanyabiashara wadogo ni gharama ya vifaa hivyo.

Baadhi yao walidai bei ya vifaa hivyo ni kubwa kwa wafanyabiashara wadogo. Uchunguzi wetu ulibaini ndoo maalumu ya kunawia mikono inauzwa kati ya Sh. 10,000 hadi 20,000, sabuni za maji zinauzwa kati ya Sh. 3,500 hadi 4,500 sokoni hapo.

Hata hivyo, Meneja wa soko alisema utaratibu waliouweka ni kutoa elimu kwa wafanyabiashara wanaozunguka soko hilo ili kila mmoja awajibike kuweka vifaa hivyo.

Alisema tangu serikali itoe maagizo kuhusu virusi vya corona na kutaka maeneo yenye mikusanyiko yote yachukue tahadhari ikiwamo kuweka vifaa vya kunawia mikono, uongozi wa soko umefanya hivyo.

Alisema kama bei ya vitakasa mikono ni kubwa, wanaweza kutumia mchanganyiko huo wa kidonge cha chloride au sabuni ya kawaida ya maji.

Pia alitaja changamoto nyingine ni baadhi ya watu ambao hawana makazi hulala sokoni, na wengine huwa ni wagonjwa.


Mbali na kwenye masoko, pia kuna tatizo katika minada, ambayo inahusisha makundi ya watu. Katika minada changamoto inatokana na kufanyika mara moja kwa wiki, hivyo kuwa vigumu kuweka utaratibu mzuri wa kuchukua hatua za tahadhari.

Kutokana na hali hiyo, tunaona kuwa mamlaka husika zinapaswa kuchukua hatua za ziada ikiwamo elimu zaidi na kutumia kupita kukagua wanaokaidi maelekezo ya serikali.

Tunawashauri wafanyabiashara katika masoko na kwenye minada kuheshimu maelekezo ya serikali ili kuepusha uwezekano wa kufungwa kwa sehemu hizo kutokana na ukaidi.

Wafanyabiashara wasikubali hatua hiyo kuchukuliwa kwa kuwa shughuli zao ni muhimu na zinategemewa na kila mtu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kondakta, abiria daladala jiongezeni na hatari corona

Na Sabato Kasika

**KUTOKANA** na tishio la virusi vya corona, hatua mbalimbali za kukabiliana nayo inaendelea kuchukuliwa na serikali, ili kuhakikisha Watanzania wanabaki salama.

Miongoni mwa hatua hizo, ni kuzuia mikusanyiko mikubwa ya watu, tamasha, semina na kufunga shule kwa muda wa siku 30, ikiwa ni njia mojawapo ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo.

Aidha, maelekezo hayo ya serikali yanawataka Watanzania kutosalimiana kwa kushikana mikono au kukumbatiana, ili kujikinga na kusambaa virusi vya corona, ambavyo ni rasmi tayari vimeshaingia nchini.

Serikali, pia haijawaacha nyuma wasafiri wa mabasi, zikiwamo daladala. Wasafirishaji wa mabasi hayo, wanatakiwa kubeba abiria kulingana na idadi ya viti vilivyomo ndani ya gari, ingawa katika sura ya pili ni mtihani, mkubwa .

Lengo la kufanya hivyo, ni kuepusha msongamano wa abiria ndani ya magari, hasa jijini Dar es Salaam, hali inayoweza kusababisha maambukizi ya virusi vya corona.

Kupitia taarifa ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra) iliyotolewa kwa vyombo vya habari Machi 19 mwaka huu, ni kwamba imefikia hatua hiyo baada ya kukutana na wadau wa usafiri na usafirishaji nchini.

Mbali na hilo, kila daladala inatakiwa kuhakikisha kuwa na dawa ya kuua wadudu mikononi, abiria wapake kabla ya kupanda gari na kunyunyiziwa dawa kila mwisho wa safari, kwa ajili ya usalama wa abiria, kondakta na dereva.

Pamoja na maelekezo hayo, bado tatizo la ujazaji wa abiria kwenye daladala bado lipo palepale, ingawa baadhi ya madereva wameanza kutii maelekezo ya kuwa na dawa za kuua wadudu mikononi mwa abiria, kabla ya kupanda gari.

Ni vyema sasa maelekezo hayo yakatelekezwa, ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza, kwa sababu tu ya uzembe wa kutozingatia mambo ya muhimu kama hayo kwa ajili ya usalama.

Zipo baadhi ya daladala jijini Dar es Salaam, ambazo kondakta wake hawaruhusu kabisa abiria kuingia ndani kabla hawajanawa dawa ya kuua wadudu na wakilazimisha anashushwa.

Vilevile, ni agizo la kuchukua abiria wachache wa kusimama, ingawa kuna ukaidi wa kuwapo magari ya yasiyo na dawa.

Pia, magari yanajaza abiria kupita kiasi, kana kwamba hakuna maelekezo ya kiserikali kwa ajili ya kuepuka usambazaji virusi vya corona.

Jambo hilo siyo la kufanyia mzaha. Ni vyema makondakta, madereva pamoja na abiria ambao bado hawajaona umuhimu huo, wakajiongeza na kuchukua hatua za haraka badala ya kusubiri kukumbwa na tatizo la mamlaka za kisheria kuwachukulia hatua sahihi.

Ni bayana makondakta wanajaza abiria, ili kupata fedha zaidi. Abiria nao wanalazimika kupanda daladala zilizojaa, ili kuwahi kwenye shughuli zao za kila siku, kutokana na hali halisi.

Ushauri wa bure, ni bora kila upande ukazingatia afya zao kwanza. Ni kweli kwamba kuna changamoto ya uhaba wa daladala kwenye baadhi ya maeneo ya Dar es Salaam, hali inayosababisha abiria kukaa vituoni kwa muda mrefu, wakisubiri usafiri.

Nitamke, hicho kisiwe kigezo cha kuwafanya abiria walazimike kujazana katika daladala moja au makondakta kuwarundika kama mizigo, huku wakijua kuwa kuna tishio la virusi vya corona.

Waige mfano wa mabasi ya mwendokasi, ambayo sasa hayajazi abiria kama siku za nyuma na yana dawa za kuua wadudu mikononi, kwa ajili ya kulinda afya za abiria na madereva kwa ujumla.

Kwa janga hili la virusi vya corona, sidhani kwamba hakuna Mtanzania asiyelielewa. Niende mbali, kuwa pia sidhani kwamba taarifa ya Latra inayolenga usalama wa abiria na wasafirishaji, ni ngeni.

Inawezekana, wapo wasioamini na hata wanadharau, wakidhani kwamba virusi vya corona havipo. Ni vyema wakatambua kuwa hili ni janga la dunia nzima, kwa hiyo suala la kuchukua tahadhari ni muhimu.

Virusi vya corona vimeshakatisha maisha ya watu katika maeneo mbalimbali duniani, lakini kwa kinachofanyika sasa kwenye baadhi ya daladala, ni kama Watanzania hawana habari kuhusu hatari ya virusi hivyo.

Waswahili wana msemo 'Ukiona mwenzio ananyolewa na wewe tia maji', hivyo wakati nchi mbalimbali zikiendelea kukumbwa na virusi vya corona, Watanzania nao hawana budi kuwa makini.

## Wadau Mahakama Kisutu wapewa mafunzo corona

**Na Hellen Mwango**

WADAU wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakiwamo waandishi wa habari, wamepatiwa mafunzo ya kujikinga na mambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona.

Mafunzo hayo yametolewa jana katika Mahakama ya Kisutu, jijini Dar es Salaam kwa kugawanywa katika makundi ya watu wachache.

Wadau wengine waliopewa mafunzo hayo ni mahakimu, askari wa jeshi la Magereza, mawakili wa serikali na wakujitegemea na polisi.

Ofisa kutoka Idara ya Afya, Manispaa ya Ilala, Sophia Ntomola, alisema wanatoa mafunzo hayo ili wanufaika wakatoe taarifa sahihi kwa jamii.

"Bado kuna taharuki mitaani, tufanye kazi kwa tahadhari, tukizingatia njia za kujikinga na maambukizi, tuendelee kuchukua tahadhari kwa jinsi tulivyojipanga, mwananchi akijihisi tofauti aende katika kituo chochote cha afya kilichopo karibu atahifadhiwa na kupata msaada wa kwenda eneo sahihi lililopangwa kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi," alisema Ntomola.

Kuhusu matumizi sabuni na koki za kunawia maji kusababisha maambukizi, alisema kwamba inatakiwa kuwa na kifungio cha kufungua kwa kiwiko ili mtu asishike, lakini kwa kufunguliwa cha kawaida mtumiaji anaweza kuchukua maji ukanyunyizia ili kupunguza lakini inatakiwa kutumia elbo ya kufungua kwa kiwiko.




Mwendesha guta, akiwa amelisheheni mabomba marefu ya plastiki kupita uwezo wa chombo, katika eneo la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mgonjwa mpya corona abainika Znz

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGONJWA wa pili wa corona ametambuliwa Zanzibar ambaye ni raia wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 27.

Raia huyo ni mke wa raia wa Ghana, ambaye aligundulika kuwa na virusi vya corona wiki iliyopita, ambaye anaendelea na matibabu katika kituo maalum kilichotengwa na serikali kilichopo Kidimni.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Waziri wa Afya, Hamad Rashid Muhammed, alisema kuwa wiki moja iliyopita mtu huyo alipimwa na akagundulika kuwa hana corona na kuwekwa karantini. Waziri Hamad Rashid alisema kuwa jana alipopimwa aligundulika kuwa na ugonjwa huo.

"Huyu mama tulikuwa tukifuatilia taarifa zake, na jana alipimwa tena na kugundulika kuwa na virusi hivyo, ambavyo ameambukizwa na mumewe," alisema Hamad.

Alisema serikali inaendelea kuwapatia huduma ili wasiwaambukize wengine.

Aidha, waziri huyo alisema pia kuna mtu mmoja kisiwani Pemba ambaye anashukiwa kuwa na corona na amewekwa katika karantini ili kuendelea kufanyiwa uchunguzi.

Waziri Hamadi alisema watu 65 wamewekwa karantini kwa siku 14 ili kuendelea kufanyiwa uchunguzi. Alieleza kuwa anasikitishwa na baadhi ya watu waliowekwa katika karantini kitoheshimu taratibu zilizowekwa.

Alisema baadhi wamekuwa wakigoma kula chakula kwa madai kuwa gharama zake ni kubwa.

Alieleza kuwa serikali imefunga milango yake haitaki raia yeyote kutoka nje ya Zanzibar kwa lengo la kudhibiti ugonjwa huo usiendelee kuenea.

Hata hivyo, alisema kuwa baadhi ya wafanyabiashara wamekua wakiuza bidhaa za kujikinga na corona ambavyo vimeshapita muda wake wa matumizi.

Alisema kuwa serikali imelifungia duka moja la dawa kwa kuuza dawa ya kunawia mikono ambayo ipo chini ya kiwango.

# Mkurugenzi General Supplies abadilishiwa mashtaka

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri umewabadilishia hati ya mashtaka Mkurugenzi wa Kampuni ya Jaruma General Supplies Ltd, Lucas Mallya na wenzake watano na kuwasomea upya mashtaka 23 ya uhujumu uchumi ikiwamo kukwepa kodi ya vileo, kuisababishia serikali hasara na kutakatisha zaidi ya Sh. bilioni 31.48.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka hayo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Godfrey Issaya.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo alidai kuwa washtakiwa hao wote wanadaiwa kusababisha hasara ya Sh. 31,489,529,153.07.

Wankyo aliwataja washtakiwa wengine kuwa ni, Happy Mwamugunda, Prochesi Shayo, Geofrey Urio, Mhasibu Tunsubilege Mateni na Mkaguzi wa Hesabu, Nelson Kahangwa.

Katika shtaka la kwanza washtakiwa wote wanadaiwa kati ya Januari 2015 na Januari 7, 2020 jijini Dar es Salaam kwa pamoja waliongoza genge la uhalifu kwa nia ya kupata faida.

Ilidaiwa katika shtaka la pili mpaka la saba linalomkabili Mallya, Juni 3, 2019 jijini Dar es Salaam, alighushi kutengeneza stempu ya ushuru akionyesha imetengenezwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wakati si kweli.

Pia ilidaiwa alitoa nyaraka hiyo ya kughushi TRA akionyesha ni halali wakati akijua si kweli na katika shtaka lingine inadaiwa Januari 7, mwaka huu, Chang'ombe 'A' Temeke Dar es Salaam alikutwa na rola 93 za stempu zenye thamani ya Sh. 80,516,000 alizozichapisha bila kibali cha Kamishna wa Mapato.

Mshtakiwa Lucas anadaiwa kati ya Januari 2016 na Desemba 31, 2019 jijini Dar es Salaam, kwa kutengeneza stempu hizo za kughushi, alisababisha hasara kwa serikali ya Sh. 15,241,075,169, akikwepa kodi kiasi hicho cha fedha na shtaka la saba anadaiwa kutakatisha kiasi hicho akijua zinatokana na zao la kukwepa kodi.

Shtaka la nane linalomkabili Happy Mwamugunda ambaye ni Mkurugenzi wa Happy Imports Associates, anadaiwa Januari 2017 na Desemba 2019, bila kusajiliwa na Kamishna wa kodi aliingiza katoni 413 za mvinyo zenye thamani ya Sh. 24,780,000 na shtaka la tisa anadaiwa kukwepa kodi ya Sh. 9,584,401,393.

Mshtakiwa huyo katika shtaka la 10 anadaiwa kipindi hicho alisababisha hasara ya Sh. 9,584,401,393 na shtaka la 11 anadaiwa kutakatisha kiasi hicho cha fedha huku akijua fedha hizo zinatokana na zao la kukwepa kodi.

Shtaka la 12 linalomkabili Proches, anadaiwa Desemba 19 mwaka 2019, alisambaza bidhaa zilizowekwa stempu za kughushi, katoni 749 za mvinyo zenye thamani ya Sh. 98,670,000, katoni 594 za mvinyo aina nyingine zenye thamani ya Sh. 12,002,000, katoni 14 za cousins 75CL14 zenye thamani ya Sh. 16,240,000 katoni za Amalura 58 zenye thamani ya Sh. 12,120,000, zote thamani yake ikiwa ni Sh. 139,032,000.

Washtakiwa hao wanadaiwa katika shtaka la 13 walikwepa kulipa kodi Sh. 38,827,276, shtaka la 14 walikwepa kulipa kodi Sh. 2,359,342,542.07 na shtaka la 15 na 16 wanadaiwa kusababisha hasara ya jumla ya fedha hizo na 17 kutakatisha.

Inadaiwa shtaka la 18 linalomkabili Urio ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya GMU group, Desemba 2018 kwa nia ya kukwepa kodi, akiwasilisha taarifa za hesabu za uongo TRA na kusababisha kukwepa kodi ya Sh. 4,265,882,773.


**BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent& Legal Consultant

**NOTISI NA TANGAZO LA MDANA**

Kwa Idhini tuliyopewa na BANK OF AFRICA (BOA) Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo huo kwa MNADA WA HADHARA.Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO |
|---|---|---|
| 1. | MAXLINE INTERNATIONAL COMPANY LIMITED | Nyumba ya makazi yenye hati na.77969, kiwanja na.2006,Kitalu "F"Iliyopo Tabata Dar es salaam kwa jina la **MAKIKO MWEMEZI MACKSON** |
| 2 | MOHAMED ABDALLAH MOHAMED | Nyumba ya makazi yenye Hati na.56851, kiwanja na.306,Kitalu'B'Iliyopo maeneo ya Mbweni Malindi manispaa ya Kinondoni Dar es salaam kwajina la **SELEMANI MASOUD MKIRITI na AMINA MOHAMEDI MKIRITI** |
| 3 | JOSEPH PETER MUSIBA | Nyumba ya makazi yenye Hati na.28542,Kiwanja na.30,Kitalu 'C' iliyopo eneo la Luchelele mjini Mwanza kwajina la **JOSEPH PETER MUSIBA** |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugezi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road.
Green Acres Buliding, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537

AU Mkurugezi Mtendaji
Bank of Africa
Head Office,
NDC Development House, ohio street-kivukoni
P.O. BOX 3054,
DAR ES SALAAM
Tel: +255-22-2110104/2111290
Fax: +255-22-2113740

156810

# BANK OF BARODA (TANZANIA) LTD.

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uonyeshaji ya Mwaka 2014)

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2019

(Kiasi kwa Shilingi milioni)

| | | MWAKA WA SASA 31.12.2019 | MWAKA ILIYOPITA 31.12.2018 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 2 955 | 3 744 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 21 842 | 17 681 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | 21 172 | 23 368 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 32 749 | 27 511 |
| 5 | Hundi na Mihamala ya Kushughulikiwa | - | 11 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 113 652 | 98 573 |
| 12 | Mali Nyingine | 3 378 | 1 412 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1 349 | 1 279 |
| 16 | **Jumla ya Mali** | **197 097** | **173 579** |
| B. | DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 5 847 | 1 272 |
| 18 | Amana za Wateja | 149 691 | 132 158 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 183 | 137 |
| 23 | Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 38 | 41 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Mihamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 36 | 20 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1 898 | 896 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **157 693** | **134 524** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **39 404** | **39 055** |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10 000 | 10 000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | 937 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 27 277 | 21 987 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1 103 | 2 147 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 1 024 | 3 984 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **39 404** | **39 055** |
| 38 | Dhima zisizo Dhahiri | 12 413 | 7 209 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 2 495 | 6 567 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 893 | 2 151 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 20% | 22% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2% | 7% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 74% | 76% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 58% | 57% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 85% | 86% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 17% | 3% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 14% | 3% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 31.12.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 31.12.2018 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 14 811 | 13 582 |
| 2 | Gharama za Riba | 4 843 | 4 676 |
| 3 | **Mapato halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **9 968** | **8 906** |
| 4 | Madeni Viza yaliyofutwa | 4 036 | 1 259 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 464 | 1 018 |
| 6 | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **1 906** | **1 932** |
| | 6.1 Faida/Hasara zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 618 | 349 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 1 278 | 1 519 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 10 | 64 |
| 7 | **Gharama Zisizo na Riba:** | **5 639** | **5 063** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 2 427 | 1 869 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 625 | 441 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 2 587 | 2 753 |
| | 7.4 Other Provision | - | - |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **1 736** | **3 498** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 634 | 1 351 |
| 10 | **Faida/(Hasara) ya Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1 103** | **2 147** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainishi)** | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **1 103** | **2 147** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | **49** | **48** |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 110 | 215 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | **4** | **4** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1% | 2% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 6% | 7% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 47% | 47% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 7% | 5% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2019

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 31.12.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 31.12.2018 |
|---|---|---|---|
| I | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 1 736 | 3 498 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | - | - |
| | -Hasara katika Mali | 685 | 1 246 |
| | -Prior Period Adjustment | (1 002) | (211) |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | (15 543) | (13 583) |
| | -Faida/Hasara kwenye Mauzo ya Mali | - | (4) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | 17 533 | 6 566 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi zilizoafikiwa | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 5 637 | (3 157) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 3 915 | 7 451 |
| | -Kodi Iliyolipwa | (634) | (1 351) |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | 110 | (400) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa(tumika) kwa Shughuli za Uendeshaji** | **12 438** | **55** |
| II | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji: | | |
| | -Gawio Lililopokewa | - | - |
| | -Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | (42) | (45) |
| | -Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | 5 |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | 2 196 | (6 035) |
| | *-Mengineyo (ainisha)* | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **2 154** | **(6 075)** |
| III | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli Kifedha: | | |
| | -Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | -Gawio Lililolipwa kwa Fedha Tasilimu | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** |
| **IV** | Fedha tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu: | | |
| | -Ongezeko/ punguzo Halisi Katika Fedha Tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu | **14 591** | **(6 021)** |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | 31 307 | 37 328 |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | **45 898** | **31 307** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2019

(Kiasi Kwa Shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya Bei ya Hisa | Mapato yaliyo Bakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineya (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MWAKA WA SASA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **10 000** | **-** | **24 134** | **3 984** | **937** | **-** | **39 055** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1 103 | - | - | - | 1 103 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 3 209 | (3 209) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | 937 | - | (937) | - | - |
| Mengineyo | - | - | (1 002) | - | - | - | (1 002) |
| Revaluation Reserves | | | | | | 249 | 249 |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10 000** | **-** | **28 381** | **775** | **-** | **249** | **39 404** |
| **MWAKA ULIOPITA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **10 000** | **-** | **22 271** | **4 068** | **781** | **-** | **37 120** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2 147 | - | - | - | 2 147 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 84 | (84) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | (156) | - | 156 | - | - |
| Mengineyo | - | - | (212) | - | - | - | (212) |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10 000** | **-** | **24 134** | **3 984** | **937** | **-** | **39 055** |

**BAADHI YA MAELEKEZO KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2019**

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za Mwaka uliopita. (Mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya /mwaka wa sasa, yaelezwe kwa mujibu wa ISA 34 na ISA 8)**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Rajendra Sadashiv Mohrir<br>(Mkurugenzi Mtendaji) | | 13th March, 2020 |
| Deogratias Edward Ndushi<br>Mkuu wa Fedha | | 13th March, 2020 |
| Mwita Mohamed Mwita<br>(Mkaguzi wa Ndani) | | 13th March, 2020 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasirishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dkt. Proches Meshili Kiwango Ngatuni<br>(Mkurugenzi) | | 13th March, 2020 |
| Dkt. Imanueli Daniel Mnzava<br>(Mkurugenzi) | | 13th March, 2020 |

215680502

# Walia kodi dagaa kupanda

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

USHIRIKA wa wauza samaki katika soko la kimataifa mwaloni jijini Mwanza (Uwasa), umeiomba serikali kupunguza kodi ya dagaa, baada ya wafanyabiashara kutoka nje ya nchi kushindwa kumudu na kuacha kwenda kununua dagaa katika soko hilo.

Mwenyekiti wa Soko hilo, Fikri Magafu, alisema jana kuwa tangu Julai mwaka jana, serikali ilipandisha kodi ya samaki hao wadogo kutoka Dola 0.16 (Sh. 368) hadi Dola 0.2 (Sh. 460) kwa kilo.

"Serikali ilipandisha kodi ya dagaa tangu mwaka jana na kusababisha wafanyabiashara kutoka nje ya nchi kushindwa kumudu na kuacha kuja kununua tena dagaa, hivyo tunaiomba ishushe kodi hiyo ili wafanyabiashara hao warudi kununua," alisema.

Magafu alisema wafanyabiashara hao kutoka nchi za Burundi, Uganda, Rwanda, Malawi, Zambia na DRC, wamelazimika kuacha kwenda kununua dagaa kwenye soko hilo na kuelekeza mitaji yao kwenye masoko ya nchi za Ethiopia, Msumbiji, Kenya na Zanzibar.

Alisema pamoja na serikali kuahidi kwa muda mrefu kushusha kodi hiyo, bado haijafanya hivyo na kwamba hivi sasa dagaa wameshuka soko lake, gunia likiuzwa kuanzia Sh. 90,000 hadi 110,000, wakati awali liliuzwa kuanzia Sh. 160,000 hadi 180,000.

"Biashara ya dagaa haina bei elekezi bali ni soko huria, kuna wakati inapanda kutokana na kuadimika lakini wakati mwingine inashuka kutegemea na nyakati hizo kuwa nyingi zaidi na kukosa wateja," alifafanua.

Alisema kwa hivi sasa, dagaa wanasafirishwa kwenda kuliwa ndani ya nchi katika mikoa ya Arusha, Mbeya na Dar es Salaaam kutokana na wanunuzi wa nje kuacha kwenda Mwanza kuwanunua.

# Polisi wawaondoa wapigadebe stendi

**Na Ambrose Mwita,** TARIME

JESHI la Polisi mkoa wa kipolisi Tarime/Rorya kitengo cha Usalama Barabarani limefanya oparesheni ya kuwaondoa wapigadebe katika stendi kuu ya mabasi yaendayo mikoani katikati ya mji wa Tarime.

Oparesheni hiyo iliendeshwa eneo hilo kuzuia tabia ya baadhi ya vijana hao ambao wamekuwa wakiwabughudhi abiria kwa kuwalazimisha kupanda mabasi ambayo wanapokea ujira.

Imeelezwa na maofisa wa polisi wanaoratibu zoezi hilo kwamba kipindi hiki ambacho taifa linachukua kila hatua ya kukabiliana na maambikizi ya virusi vya corona mamlaka wilayani hapa zinafanya kila ziwezalo kujaribu kupunguza msongamano katika maeneo ya mikusanyiko ikiwamo stendi na masoko.

Kwa mujibu wa mkuu wa kitengo cha usalama barabarani Tarime/Rorya, Ally

Shaali, wamiliki wa mabasi wanaotumia stendi hiyo wanatakiwa kufuata sheria za barabarani bila shuruti ikiwamo kuepuka kujaza abiria kuliko uwezo wa vyombo vyao vya usafiri.

"Hatua kali zitachukuliwa kwa madereva ambao watashindwa kutimiza vigezo vya kiusalama na afya kabla ya kuanza safari zao ikiwa ni pamoja na kuhakikisha abiria wanakaa kwa usalama bila kuzidisha zaidi ya uwezo wa viti vilivyomo katika mabasi yao," alisema Shaali.

Alisema wapigadebe wamekuwa wakisababisha usumbufu kwa abiria na watumiaji wengine wa vyombo vya usafiri hususan katika maeneo ya stendi huku katika baadhi ya nyakati wakilazimika kuwagusa na kung'ang'ania mizigo yao, hali inayopaswa kuepukwa katika kipindi hiki cha maambukizi ya corona.

Katika hatua nyingine, Jeshi hilo limeendesha msako wa kushtukiza kabla, wakati na baada ya safari katika vyombo vyote vya usafiri vikiwamo vya binafsi ili kuhakikisha wanatekeleza utii wa sheria za barabarani na kiafya kama ilivyoelekezwa na serikali kupitia Wizara ya Afya. Hivi karibuni mfanyabiashara maarufu wilayani hapa na Mkurugenzi wa

Kampuni ya mabasi ya Zacharia, Peter Zacharia, aliomba kuondolewa wapigadebe katika stendi hiyo kutokana na baadhi yao kujihusisha na kusababisha usumbufu na wakati mwingine kupotea mizigo ya abiria.




Meneja mradi wa kifua kikuu wa shirika lisilo la kiserikali la Shdepha+, Mwinuka Ereneus (wa pili kushoto) na Mratibu uhakiki na tathimini, Rabia Abeid wakiwa wameshika bango lenye ujumbe "Linda afya ya mapafu yako dhidi ya kufua kikuu" kama sehemu ya maadhimisho ya siku ya kifua kikuu Duniani, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wafanyabiashara watakiwa kujiunga huduma bima afya

**Na Boniface Gideon, KILINDI**

WAFANYABIASHARA wa Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, wametakiwa kujiunga na bima za afya ili kuwa na uhakika wa matibabu.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Mkoa wa Tanga, Ally Mwakababu, wakati akitoa elimu juu ya faida ya kujiunga na bima za afya kwa wafanyabiashara wadogo maarufu kama 'machinga'.

Mwakababu alisema mwanzo wananchi walikuwa na dhana kuwa mifuko ya bima za afya ilikuwa ni kwa wafanyakazi walioajiliwa.

"Tumekuja kuwaambia kuwa bima ya afya ni kwa watu wote na sio waajiliwa pekee...tunawapa elimu wafanyabiashara kuwa ili uweze kuendeleza biashara yako na usifirisike, ni lazima uwe na uhakika wa matibabu," alisema Mwakababu.

Alisema familia nyingi zimeingia kwenye matatizo kutokana na gharama kubwa za matibabu.

"Sasa hivi tuna fao la jipimie, ndio maana tumekuja kuzungumza na nyie wananchi kuwa matibabu ni gharama kubwa, hivyo ni vyema mkajiunga na bima ya afya, " alisema Mwakababu.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kilindi, Bakari Mkalakala, aliwaomba wadau na watumishi wa umma kuhakikisha wanashirikiana na wananchi katika utoaji wa elimu juu faida ya kujiunga na bima za afya.

Alisema CCM katika wilaya wamejipanga kuendelea kuwaelimisha wananchi juu ya faida ya kujiunga na NHIF.

"Niwaombe viongozi wa CCM wilaya yetu kuanzia ngazi za chini muwaelimishe wananchi juu ya faida ya kujiunga na bima za afya na mimi nitazunguka kutoa elimu hii," aliongeza Mkarakala.

Baadhi ya wafanyabiashara walishukuru serikali kwa kuwafikia wananchi wa maeneo ya vijijini kupata elimu juu ya faida za bima ya afya.

"Tunashukuru sana kwa hili la kuletewa elimu hii, sisi tulioko huku vijijini hatujawahi kufikiria kwamba tutakuja kufikiwa na huduma hizi... ila tunaomba gharama za bima zipunguzwe kidogo ili sisi wanyonge tumudu," alisema Salehe Mhina.

# EAC kusambaza magari kuchunguza wagonjwa corona

**Na Novatus Makunga,**
ARUSHA

JUMUIYA ya Afrika ya Mashariki (EAC) ipo katika hatua za mwisho za kusambaza magari maalumu yenye maabara ya kupima na kuchunguza ugonjwa wa homa ya virusi vya corona katika nchi wanachama wa jumuia hiyo.

Taarifa iliyopatikana jana jijini hapa kutoka makao makuu ya Sekretarieti ya Jumuiya hiyo, imeeleza kuwa kila nchi itapewa gari moja lenye uwezo wa kupita kwenye barabara mbovu likiwa limefungwa vifaa vyote vya kupima virusi hivyo na pia ugonjwa wa ebola.

Pia, Sekretariati hiyo imeunda kamati ya uratibu ya eneo hilo RCC ambayo itajikita zaidi kutengeneza mawasiliano ya dharura katika jamii, sera, usimamizi pamoja na takwimu kwa lengo la kufuatilia kwa karibu ugonjwa wa homa ya virusi vya corona (Covid-19).

Tayari kamati hiyo imeanza majukumu yake kwa kuhakikisha vyombo vyote vya jumuiya hiyo vinashiriki kikamilifu katika mapambano.

Katika hatua nyingine Sekretariati ya EAC imeandaa mkutano maalumu wa mawaziri wanaohusika na masuala ya afya ambao utafanyika kwa njia ya video kwa lengo la kutajadili mikakati ya kuzuia na kusambaa kwa ugonjwa huo katika eneo hilo.

Mkutano huo ulifanyika jana, huku nchi nne kati ya sita wanachama wa jumuiya hiyo zikiwa tayari zimeshakumbwa na maambukizi ya ugonjwa huo.

Baadhi ya nchi wanachama zimeshachukuwa hatua za kitaifa ndani ya nchi zao zikiwamo kuzuia mikutano na mikusanyiko yote, kufunga shule na taasisi nyingine za taaluma na mafunzo pamoja na kuzuia safari zote za nje za ndege pamoja na njia za barabara.

Vile vile, nchi hizo pia zimeweka utaratibu maalumu wa kuwaweka katika karantini wasafari wote wanaowasili kutoka katika nchi ambazo tayari zina maambukizi ya ugonjwa huo.

Nchi nne za EAC zenye maambukizi ya virusi vya corona ni pamoja na Kenya yenye wagonjwa 15, Rwanda (17), Tanzania (12) na Uganda mgonjwa mmoja.

Nchi nyingine mbili za Burundi na Sudan Kusini hadi jana asubuhi hazikuwa na mgonjwa.

Nchi jirani na Afrika ya Mashariki za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Somalia zote zina mgonjwa mmoja mmoja.



Baadhi ya watu waliokamatwa eneo la Loliondo, wilayani Ngorongoro mkoani Arusha wakidaiwa kuwa ni wahamiaji haramu wakiingia kwenye gari tayari kwa kupelekwa mahakamani, juzi. Jumla ya watu 37 wamekamatwa na 12 wameshafikishwa mahakamani na wengine wanaendelea kuhojiwa. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# 'Ulaji vitu vigumu hatari kwa meno'

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

ULAJI wa vitu vigumu umetajwa kuwa ni hatari kwa afya ya kinywa na meno na kuwa chanzo cha meno kulegea.

Hayo yalisemwa jana mkoani Manyara na Mkuu wa Kitengo cha Afya ya Kinywa na Meno wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Edward Magoma wakati akizungumza na Nipashe.

"Ni kweli kuna watu wanakula vitu vigumu mfano mtu anafungua soda kwa kutumia meno hiyo ni hatari," alisema Dk. Magoma.

Alisema ulaji wa miwa migumu na barafu ni tatizo kwa afya ya meno. "Barafu ikiwa ngumu inaweza kuharibu meno na jino likipata presha linalegea na hatimaye mhusika kuanza kuhangaika na kutafuta matibabu," alisema. Mkazi wa Babati Charles Simon, alikiri baadhi ya watu kutumia meno kufungua vizibo vya soda bila kujua madhara yake kiafya. Alisema watu wengine wanafanya vitu kwa mazoea, lakini baadaye vinaleta shida na kuathiri uchumi wa familia zao.

"Hapa inatakiwa elimu itolewe kwa wazazi ambao wengi wetu yumekuwa tunawanunulia barafu watoto wetu tukidhani upendo kumbe tunawapa ugonjwa," alisema Charles.

Mkazi wa Gendi, Winifrida Tluway, aliishauri serikali kuwa inatuma timu ya wataalamu wa meno vijijini ili jamii ipate elimu na kuepuka madhara.

## Apiga 'stop' machinga kutozwa 500/- za usafi

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni, amepiga marufuku viongozi wa soko la madini la jijini humo, kutoza Sh. 500 wafanyabiashara wadogo wa madini (machinga) kwa ajili ya usafi.

Akitoa agizo hilo jana alipotembelea soko hilo, Dk. Madeni alisema, kitendo cha kutoza wafanyabiashara hao fedha hizo ni kwenda kinyume na agizo la Rais John Magufuli la kuzuia machinga kutozwa ushuru.

"Mimi nimepata malalamiko toka kwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, kuwa katika soko hili mnatozwa ushuru na Mwenyekiti wa soko hili, Abugasti Mollel, kwa ajili ya usafi, kuanzia sasa 'stop' kama usafi nitaagiza kampuni iliyopewa tenda ya kuzoa taka katika jiji hili, ili waje hapa sokoni kila siku kuchukua takataka, sitaki kusikia watu wanatoza fedha,"alisema.

Alisema fedha zinatozwa kwa kutoa risiti za kawaida na siyo za elekroniti (EFDs), jambo ambalo halikubaliki.

Alimuagiza mwenyekiti huyo (Abugasti) kuwa makini na kuifahamu mipango ya baadhi ya wanasiasa ambao wana malengo yao ndani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) au nje ya chama hicho ya kumuharibia Mkuu wa wilaya aonekane hafai katika kazi, kwa kutoa maelekezo yalio tofauti na maagizo ya Rais Magufuli.

Hata hivyo, alisema kitendo cha kutoza wafanyabiashara hao fedha hizo, ilikuwa amfunge pingu na kumpeleka mahabusu, lakini kwa sababu alikiri kutoza watu fedha hizo kwa maelekezo ya Kamishna wa Madini wa mkoa huo (RMO), Hamisi Kamando, alimsamehe.

Kwa upade wake Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, alimuagiza Mkurugenzi Dk. Madeni kutembelea soko hilo na maeneo yote yenye malalamiko na machinga kutozwa ushuru na kushughulikia haraka changamoto hiyo.

"Mimi nimepokea malalamiko toka kwa baadhi ya machinga wa soko la madini Arusha, wakilalamika kutozwa Sh. 500 kwa ajili ya usafi wa soko hilo, hiki kitendo ni kinyume na agizo la Rais, sasa naomba mkurugenzi nenda kwenye soko hilo ukapige 'stop' uchangishaji wa fedha hizo," alisema.

Pia aliwaomba machinga hao kuacha kutumika kisiasa na hasa mwaka huu wa uchaguzi mkuu na kuhakikisha wanampa kura mtu aliyehangaika nao.

## Taasisi za umma zafeli upandaji miti

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

TAASISI za umma zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, zimetajwa kushindwa kufikia lengo lililowekwa na serikali la upandaji wa miti kila mwaka.

Hali hiyo imeelezwa kuharibu mikakati yake ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Hayo yamo katika waraka maalum wa Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Costantine Kanyasu, alioutoa kwa Mmnejimenti ya Shamba la Miti la Taifa la West Kilimanjaro.

Katika waraka huo, Kanyasu alisema taasisi nyingi zikiwamo baadhi ya halmashauri za wilaya zimeshindwa kufikia lengo la kupanda miche ya miti 1,500,000 kila mwaka ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabiachi na uharibifu wa mazingira. "Nilipotembelea shamba la bustani ya miche ya miti katika Shamba la Miti la Taifa la West Kilimanjaro lililoko Wilaya ya Siha, nimekuta bado kuna tatizo kama hilo na nimetoa maelekezo ya kufuatwa kuanzia sasa. Hatuwezi kuzifumbia macho taasisi za umma ambazo zitashindwa kufikia lengo.

Kanyasu aliongeza: "Kama serikali tutajitahidi sana kutafuta ufumbuzi wa mlipuko wa ugonjwa mbaya unaoshambulia miche inayotokana na miti ya kupandwa katika shamba hili. Hata hivyo, wataalamu wetu wanasema ugonjwa huo uliolipuka wa kuozesha miti hiyo unafahamika kama 'dumping off'."

Pia katika waraka huo, amezitaka halmashauri za wilaya kushirikisha taasisi za elimu katika kampeni za upandaji miti.

Kwa mujibu wa Kanyasu, miti inayokatwa kwa ajili ya shughuli za kibinadamu nchini ni mingi, ikilinganishwa na miti inayopandwa, ambapo hekta 470,000 za miti zinakatwa kila mwaka.

Alipotafutwa kuzungumzia kauli ya Naibu Waziri huyo, Meneja wa shamba hilo, Magesa Mabego, alisema wanashindwa kufikia malengo ya upandaji miti kwa mwaka kutokana na changamoto ya ukame, wananchi kuvamia maeneo ya msitu pamoja na magonjwa yanayoshambulia miche ambayo wameshindwa kuipatia ufumbuzi.

Msimamizi wa bustani ya miche katika shamba hilo, Devota Bura, alipoulizwa kuhusiana na tatizo hilo, alisema kushindwa kwao kufikia lengo kunatokana na kuibuka kwa ugonjwa wa miche kuoza katika kitalu cha miche na hatimaye huamia kwenye kitalu kwenda kwenye viriba.

"Unaweza kuotesha miche 50,000 ikakua miche 35,000, huku miche 15,000 yote ikawa imeshambuliwa na ugonjwa huo na kufa. Tumejitahidi kupiga dawa lakini imeonekana bado ugonjwa huu unashambulia miche, hali ambayo inasababisha kutofikia malengo tunayokuwa tumejiwekea kwa mwaka mzima," alieleza Bura

# RC atoa maelekezo huhusu wageni walioingia kupitia KIA

**Na Godfrey Mushi, HAI**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, ameagiza wageni 15 walioingia mkoani humo kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) kuwekwa karantini ya hiari kwa siku 14.

Wageni hao ni wale waliokuwa wakitokea Bara la Ulaya kuja nchini kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

Mghwira alitoa maelekezo hayo jana alipotembelea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), uliopo Wilaya ya Hai. "Nimeshaelekeza mamlaka zetu ambazo ni idara ya afya pamoja na watu wa msalaba mwekundu washirikiane kutoa elimu kwenye zile hoteli ambazo wageni hao watakwenda kulingana na taratibu za kuhudumia wageni katika mfumo wa karantini.

"Kuna wageni ambao watashuka labda watafikia kwenye familia, zile familia zitapewa mafunzo pia jinsi ya kuishi nao na kuwahudumia mpaka tutakapothibitisha baada ya siku 14 kwamba hawana maambukizi. Utakwenda kuwekwa kwenye karantini ya hiari ambako ni mahali pazuri pa kuishi."

Juzi, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliwaagiza wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa na wakuu wa wilaya kubainisha hoteli za gharama ndogo ili wanaoingia nchini kutoka nchi zenye maambukizi ya virusi vya corona waweze kumudu na kukaa karantini kwa siku 14.

Ummy alilazimika kutoa maelekezo hayo, baada kuibuka malalamiko ya baadhi ya wageni kuwa wanapelekwa kwenye hoteli zenye bei kubwa, hali inayosababisha kushindwa kumudu gharama. Machi 24, mwaka huu kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter, Ummy alisema, "Tumepokea hii changamoto ya sehemu zilizobainishwa kwa ajili ya siku 14 za wasafiri waliotoka nchi zilizoathirika zaidi na virusi vya corona kukaa. Nawaelekeza ma RC (Wakuu wa Mikoa) na RAS wa Mikoa yote (Makatibu Tawala wa mikoa) kubainisha hoteli na sehemu ambazo wasafiri wengi watamudu gharama."



Baadhi ya wachuuzi wa samaki wa Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wakiuza samaki waliowavua baada ya bwawa la Kidawash kufurika juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Askofu Shoo aomba uwekezaji SMMUCo

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amewataka waumini wa kanisa hilo na watu wenye nguvu kiuchumi kutosita kuongeza nguvu katika uwekezaji wa majengo ya kisasa na miundombinu ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Askofu Stefano Moshi (SMMUCo).

Wito huo wa Dk. Shoo, unalenga zaidi kukiboresha chuo hicho katika suala la majengo, miundo mbinu na rasilimali watu ili kutimiza matakwa ya Kamisheni ya Vyuo Vikuu nchini (TCU) ya vyuo kujitanua na kuwa na hadhi ya kimataifa.

Alikuwa akizungumza jana na viongozi wa Usharika wa Lyamungo Sinde uliopo Jimbo la Hai la Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT, baada ya kuchangisha kiasi cha Sh. milioni 2.7 za uboreshaji wa chuo hicho.

"Ni lazima kama kanisa na Dayosisi ya Kaskazini, tujitahidi sana mwaka huu kukiweka chuo chetu katika hadhi ya kisasa ili kukitangaza zaidi kitaifa na kimataifa, niwaombe sana muendelee kuchangia hasa ndugu zangu mliojaliwa uwezo wa kiuchumi msirudi nyuma kutusaidia katika jambo hili,"alisema Dk. Shoo.

Desemba 25 mwaka jana, Askofu Dk. Shoo, alitangaza uamuzi wa Dayosisi hiyo wa kusimamishwa kwa michango ya mingine ya miradi ya kikanisa kuanzia mwaka 2020 katika Dayosisi ya Kaskazini ili kuruhusu fedha zitakazochangwa zitumike kukiboresha SMMCo.

Dk. Shoo ambaye pia ni Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini, alitangaza neema nyingine kwa waumini wake, baada ya kuridhia kuongeza ufadhili wa masomo kutoka wanafunzi watatu hadi sita kutoka kwenye sharika zake kuanzia mwaka wa masomo 2020/21.

Dayosisi hiyo ilitangaza mwanzoni mwa mwezi huu kuanza kutoa ufadhili huo wa masomo katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Stephano Moshi (SMMUCo) katika ngazi ya cheti na stashada.

Kozi zilizopata ufadhili huo ni fani za Maendeleo ya Jamii, Uhasibu, Uandishi wa Habari na Usimamizi wa Biashara.

# ama

ALHAMISI MACHI 26, 2020

AFYA NA MAZINGIRA





**Corona yaipa umaarufu sinema ya zamani**

Ukurasa 14



Hamahama holela ya wafugaji inavyoachia watoto janga afya

Ukurasa 16



**Mama wa mwenye ualbino asimulia majaribu ya mkunga**

Ukurasa 20




# Corona inavyozidi kuitesa dunia

Ukurasa 18




Picha ya sinema Contagion na waigizaji wake. **PICHA: MTANDAO.**

# Corona yaipa umaarufu sinema ya zamani

**Na Mwandishi Wetu**

FILAMU ya Contagion iliyotolewa mwaka 2011 na kupata umaarufu kiasi chake, ghafla sasa imekuwa na mvuto mkubwa ikiangaliwa kwamba, imebashiri mlipuko wa maradhi corona.

Contagion, iliyotengenezwa na studio ya Warner Bros. - studio imerejea ghafla kwenye orodha ya filamu zilizopakuliwa nchini Marekani na inafuatiliwa sana, bada aya kuwapo taarifa ya mlipuko wa ugonjwa huo nchini China .

Sababu kuu inatajwa ni kwamba, maudhui yake yanafanana sana na mlipuko wa corona, hasa katika nafasi ya mfanyabiashara mwanamke anayeonekana akiuliwa na ugonjwa wa ajabu, virusi alivyopata alipokuwa safarini nchini China.

Uhusiano huo na China, ni mojawapo ya mambo yanayoendana na uhalisi wa corona, mcheza filamu mwanamke wa Kimarekani aliyetuma akiwa amevalia barakoa katika ndege iliyokuwa ikisafiri kuvuka bahari ya Pasifiki .

Mcheza filamu anazungumzia mambo kama vile haja ya watu wasishikane mikono na kunawawa kila mara, jambo, ambalo ndilo limetawala masharti ya kusambaa korona

Kimsingi, ugonjwa wa corona umeanzia nchini China miezi kadhaa iliyopita na kusambaa kwingineko duniani, ikiwamo nchini Tanzania na moja ya masharti ya kukabliana nayo, ni kupepuka kupeana mikono, kunawa na utumaji barakoa katika mazingira hatarishi.

## MAZINGIRA

### MAGEUZI SIHA...

# Hakuna mgawo, maji yanapatikana ndoo ya lita 20, kwa bei shilingi 10

## Kutoka safari ndefu dhiki ya maji

**Na Mary Mosha, SIHA**

NI miaka takribani 20 sasa, tangu kuachwa shilingi 10 ya Tanzania kutumika kununua vitu mbalimbali, ikiwemo peremende. Leo, maeneo mengi hayana nguvu ya kufanya chochote katika ununuzi wa vitu, huku baadhi ya watoto wa vizazi vya sasa hawatambui kabisa.

Shilingi hiyo yenye muonekano wa sarafu ya shaba, zamani ilipokuwa na nguvu, ilikuwepo shillingi 10 ya noti iliyotumika katika ununuzi.

Hali ya sasa na kwa wenye vilivyopo sasa, ni vigumu kuifahamu. Ila, unapoenda wilayani Siha,kuna maajabu ya nguvu ya kiasi hicho cha fedha na mtu akiwa na kiasi cha shilingi 10, anajipatia maji lita 20.

Nipashe hivi karibuni ilitua katika kijiji cha Kiruwa , kwenye Kata ya Lawate, wilayani Siha na kukutana na mkazi Nicholaus Msalo, anayeanza kwa majigamho kwamba wilaya haina changamoto ya maji vijijini, kutokana na serikali kuanzisha utaratibu maalumu wa upatikanaji maji kupitia bodi za maji zilizoundwa.

Anasema, katika miaka ya hivi karibuni, walikuwa wanakabiliwa na ukosefu wa maji safi na salama na ikawalazimu kuchota katika makorongo ambayo hayakuwa safi na salama, hali iliyowaingiza katika mlipuko wa maradhi ya tumbo.

"Serikali kupitia Bodi ya Maji ya Makiwaru Magadini na Fuka Lawate, zilisaidia katika kuwezesha kutatua changamoto kubwa iliyowakwamisha wananchi wengi katika kupata maendeleo," anasema.

Mkazi mwingine, Nora Lyimo, anasema bodi hizo za maji ziliweza kumsaidia mwananchi asitembee umbali mrefu na badala yake ajikite katika shughuli za maendeleo.

"Mimi kama mama kwa sasa naweza kujikita katika kuhakikisha nashiriki katika shughuli za kimaendeleo badala ya kuanza kutembea umbali mrefu katika kuleta maji," anasema

Amina Mhando, ni mmoja ya wanaouza maji katika vilula hivi, anasema mwanzoni waliteseka sana kupata maji safi na salama tulikuwa tunapata magonjwa ya mlipuko kama homa ya matumbo.

Pia, mkazi huyo anakumbusha kwamba, walipata matatizo makubwa ya kiafya yaliyosababisha kupoteza pesa nyingi kwa ajili ya matibabu.

Inawezekanaje?

Wenyeviti wa bodi za maji zinazotoa huduma katika wilaya hiyo ya Siha, kuanzia na Mwenyekiti Yohana Laizer, wa Bodi ya Lawate Fuka, anasema katika miaka ya 1970 hadi 1980 miradi hiyo yote ilikuwa chini ya Mkandarasi wa Wilaya ya Hai.

Laizer anasema, wiliaya hiyo baadaye haijagawanjwa na kupatikana wilaya mpya ya Hai, ikiwa na miradi 15 ikiwa chini ya Mhandisi wa Mkoa.

Anaeleza kwamba, mirani hiyo ili shindwa kuendelea kutokana na ukosefu wa fedha za kufanya matengenezo na kuajiri wataalamu wa kuiendesha.

Mwenyekiti huyo anaeleza kuwa, katika mwaka 2002/2003, mradi uliweza kufanyiwa ukarabati na kupanuliwa na serikali ya Ujerumani kwa kushirkiana na serikali ya Tanzania, ikigharimu zaidi ya Sh. bilioni 3.6.

"Sehemu ya pili ya mradi huo ni Levishi ambao uligharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.7, katika vijiji vya Mese, Ngaroni, Mowo, Njamu, Samaki maini, Nrao, Kisangara, Nsherehehe,

**Inaendelea Uk. 15**



Kilula cha Lawate Fuka, ambacho wananchi walijenga uzio baada ya kuwekewa bomba la maji. Picha nyingine za huduma hiyo na wakazi wakifaidika.

**"Serikali kupitia Bodi ya Maji ya Makiwaru Magadini na Fuka Lawate, zilisaidia katika kuwezesha kutatua changamoto kubwa iliyowakwamisha wananchi wengi katika kupata maendeleo," anasema.**



MAZINGIRA

Inatoka Uk. 14

# Hakuna mgawo, maji yanapatikana ndoo ya lita 20, kwa bei shilingi 10


Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Fuka Lawate, akizungumza na mwananchi kuhusu huduma ya maji, Lawate. **PICHA ZOTE: MARY MOSHA.**

Ngirinyi na Koboko,' anafafanua.

"Mradi huo ulilenga kuwafikia wananchi zaidi ya 42,000 ifikapo 2015, ingawa hadi mwaka 2014 wananchi 41,850 walifikiwa na maji safi na salama," anasema Laizer.

Katika miaka 12 ya kuwepo mradi, unaelezwa kufanikiwa kuwahudumia maji bila ya mgawo kwa wananchi hao.

**Meneja Mradi**

Meneja wa mradi huo, Elihuruma Masaoe, anasema kuwapo mradi, kumechangia maisha kuboreka kwa kuwa na nyumba za kisasa, umasikini nao kupungua, shughuli nyingi za kiuchumi kuibuka, ufaulu wa wanafunzi shuleni kuwepo na watu 26 kuajiriwa katika mradi.

Katika suala la uendeshaji mradi huu una wajumbe za bodi, wajumbe wa kwanzia ngazi za vijiji, hadi wilaya za kamati za maji hali ambayo wameona umuhimu wa uwepo wa vilula zisivyozidi mita 400 na kuviboresha kwa kuondokana na uzio wa majani na kujenga uzio wa matofali ya kuchoma.

Kutokana na ubora wa maji yanayotolewa na bodi za maji zilizopo Siha, kumechangia kupungua kwa magonjwa ya mlipuko, ingawa bodi hiyo ya Fuka Lawate, inakabiliwa na changamoto mbalimbali, zikiwemo ongezeko la watu, mabadiliko ya tabianchi yaliyochangia, kukauka kwa baadhi ya vyanzo vya maji, ikiwemo mto Mese.

Anasema, kumekuwapo ukataji miti ya asili kwenye hifadhi ya msitu wa Kilimanjaro pamoja na maamuzi ya kujenga taasisi kubwa za kiserikali na za binafsi bila kushirikisha bodi hizo.

Julius Moleli, ni Mwenyekiti wa Bodi ya Maji Magadini Makiwaru, anasema mradi natoa huduma kwa wananchi kwa mfumo wa mita na kuna vilula (public tabs) zaidi ya 313 vinavyotoa huduma ndani ya mita 400, pia wateja 3012 wamefungiwa na kuna taasisi 400 jumla yao 3425.

Anasema, kuwa wateja wa vilula 750 kwa mita ya ujazo lita 20 kwa 15 tu, taasisi shule za msingi na sekondari, taasisi za dini, hospitali na vituo vya afya bei ya maji ni Sh.12 kwa ndoo ya ujazo wa lita 20.

Masaoe, wateja wa majumbani ni Sh. 900 kwa mita, wafanyabiashara, waosha magari na vyenye viwanda vidogo vidogo 1000 kwa mita.

"Mradi huu unaweza kujiendesha bila ruzuku ya serikali au wafadhili tangu ulipoanzishwa hadi sasa na walengwa wanatambua, mradi huo hulipa ankara zao kwao za maji kwa wakati kwa asilimia zaidi ya 97 ambapo shule zaidi ya 32 za msingi na nane za sekondari katika eneo la mradi," anasema

Anasema, mradi huo unahudumia skimu za umwagiliaji nne, ikiwemo Gararagua inayohudumia wakazi zaidi ya 22,000, sikimu ya pili Rozylin/ Mjimwema, inayotarajia kuhudumia watu zaidi ya 6000 na ya tatu ikiwa ni Lemosho (West Kilimanjaro) yenye uwezo wa kuhudumia watu zaidi ya 19,000 na ya nne ni North west Kilimanjaro unaotarajiwa kuhudumia watu 15,000.

Pamoja na mafaniko ya mradi, bado unakabiliwa na changamoto mbalimbali, zikiwamo ongezeko la maji katika skimu ya umwagiliaji ya Magadini, ambayo kwa sasa ina idadi ya watu 40,000 wakati mradi huo, ulisaini kuwa na watu 22,000 ifikapo 2015.

Anasema, kutokana na changamoto hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Siha, kwa kushirikiana mradi kuongeza tanki la maji kwa ajili ya kuongeza skimu ya Gararagua na kulaza bomba jipya lenye urefu wa kilomita 6.5.

**DC wa Siha**

Mkuu wa Wilaya Siha, Onesmo Buswelu, anasema utekelezaji huo umekuwa rahisi, baada ya bodi hizo za maji kushirikiana na serikali katika kuwafikia wananchi.

"Katika wilaya ya Siha kuna bodi mbili za maji ambazo zinashirikiana na serikali katika kuwahudumia wananchi, hali iliyosaidia kufikisha maji kwa wananchi kwa asilimia 87.

"Hivyo, tumevuka malengo yaliyowekwa na wizara ya vijijini kufikishe maji kwa asilimia 85, "anasema Mkuu wa Wilaya, Biswelu.

Aidha, mkuu huyo aliwataka wananchi kutunza vyanzo vya maji pamoja na miundombinu, iliyowekwa na miradi hiyo, ili waweze kupata maji bila ya mgawo

Pia, kiongozi wa kisiasa - CCM, Wilfred Mosi, anasema katika wilaya hiyo imewasaidia wananchi kupata maji kwa vijiji 60, ingawa bado kuna vijiji 12 hawapati maji ya kutosha, ingawa serikali imechukua jukumu na kushirikiana na bodi katika kuhakikisha wanamtua mama ndoo kichwani.

"Katika wilaya hii kunamiradi ya maji miwili ya Fuka Lawate na Magadini Makiwaru, iliyosaidia kumtua mama ndoo kichwani ambayo kwa kushirikiana na serikali na kusambaza maji kwa asilimia 85 kwa vijijini," anasema Mosi.

AFYA

# Hamahama holela ya wafugaji inavyoachia watoto janga afya

## •Msimu ukifika wanatelekeza chanjo
## •Halmashauri yalia nao 'itakuwaje ?'



Wafugaji na wakulima wa wilaya ya Meatu wakijianda na safari kuelekea mikoa mingine. **PICHA: HAPPY SEVERINE.**

**Na Happy Severine, Meatu**

KUNA shida ya matibabu kwa watoto kutoka jamii za wachungaji wilayani hapa. Kama ilivyowahi kuripotiwa na gazeti hili, hamahama ya jamii hiyo kwenda kutafuta malisho inavyoathiri elimu, hilo nalo ni janga kwa huduma ya afya.

Hadi sasa inaelezwa, wakazi wa Meatu, wameshindwa kudhibitiwa katika mwenendo huo, hata kuzua madhara makubwa kwa watoto wengi, wahusika wakuu ni familia za wafugaji.

Namna madhara yalivyo, inaelezwa muda mrefu wanakosa huduma za msingi za afya watoto wao, ikiwamo chanjo mbalimbali zinazotolewa kwao, pia wajawazito.

**SERIKALI YAONGEA**

Charles Manota ni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mwamanimba, anataja sababu kubwa ya wananchi kuhama kila mwaka, ukame unaoikumba wilaya hiyo, hata inasukuma watu kuhama kwa kukosa mashamba ya kilimo, wakielekea mikoa ya Morogoro, Katavi, Rukwa na Tabora.

> **"Elimu itolewe zaidi kwani kuhama siyo jambo baya, lakini mtoto akienda na taarifa zake muhimu, hata huko ambako anaenda ataendelea na huduma hizo hizo vizuri. Ni elimu tu inahitajika kwa wingi," anasema Jilala.**

Ofisa Mtendaji huyo anaeleza hilo, zaidi linatokea katika miezi Julai, Agosti, Septemba, Oktoba hadi Novemba, makundi makubwa ya wananchi wanakimbia, kusogelea mikoa hiyo.

Manota anabainisha moja ya eneo ambalo watoto wadogo wamendelea kukosa haki hizo za msingi kwenye wilaya hiyo, ni katika kata ya Mwamanimba, ambayo mwaka jana kaya nyingi zilihama.

Manota anataja sekta inayoathiriwa zaidi na hamahama ya wananchi wilayani, ni afya ambayo watoto na wajawazito wengi wanakuwa hawajamaliza chanjo na dawa za kinga mbalimbali.

Analalamika serikali imekuwa ikitumia pesa nyingi kunusuru vifo vya watoto wachanga na wajawazito, kwa kuanzisha chanjo kama kinga kuu na kuwahudumia kwa karibu wajawazito, lakini ni tofauti kwa jamii ya ufugaji.

> **" Hata kama tatizo ni ukame, tunawaambia kutoa taarifa ni muhimu na watoto wawachukulie uhamisho, lakini wengi hawajali hilo, na sisi kuwafuatilia hatuna uwezo huo kwani kunahitaji gharama kubwa," anasema Jilala.**

Mganga Mfawidhi wa zahanati ya kijiji cha Mwamanimba, Victor Moshi, anasema kwa chanjo za watoto wenye umri chini ya miaka mitano wanaathirika zaidi, kwani wengi hawamalizi dozi kutokana na wazazi wao kuhama

Moshi anasema, serikali imekuwa ikitoa chanjo ya kutibu maradhi ya tumbo, kifua kikuu, pepopunda, kifaduro, pumu, surua, lubera na polio, kwa ajili ya kuwakinga watoto wadogo.

Anasema, inawakinga watoto hao na maradhi ili wasipatwe na magonjwa, lakini watoto hao wa wafugaji wamekuwa wakikatishwa kupata huduma hizo.

Moshi anasema, mwaka jana familia nyingi zilihama katika kijiji hicho, malengo yao yalikuwa kuwafikia watoto 324, lakini waliopata



Watoto wakipatiwa huduma za chanjo. **PICHA; MTANDAO.**

chanjo kwa usahihi ni asilimia 64 ya malengo.

"Wengi wamehama na wazazi wao, hakuna mzazi hata mmoja ambaye amekuja kuaga ili tuweze kumwandikia barua ya kumtambulisha mtoto wake kule anakokwenda, ili wajue amepata chanjo gani kwa kiasi gani na aweze kuendelea," anasema Moshi.

Pia, anasema kuwa asilimia zaidi ya 30 ya watoto hao hawajamaliza chanjo husika, hivyo wana hatari katika siku za baadaye kupata magonjwa hayo na yakawaletea matatizo zaidi ikiwemo vifo.

Anasema, wamekuwa wakifanya jitihada kubwa ya kuwaelimisha wananchi umuhimu wa wajawazito na watoto kupata chanjo zote kwa wakati, lakini jamii hiyo ya kifugaji bado haijaona umuhimu unaosisitizwa.

"Binafsi naumia sana pale ninapoona watoto wadogo na wajawazito wanashindwa kupata chanjo wa uzembe, wakati serikali inajitahidi sana kuboresha huduma zao," anasema.

Moshi anaiomba serikali ya wilaya na kata kwa umoja wao, kutafuta namna sahihi ya kuwajengea mazingira mazuri wafugaji, ili wafuge kisasa na kuachana na tabia ya kuhama, hali inayoyumbisha maisha ya familia zao

Kwa mujibu wa Moshi, mwaka jana idadi kubwa ya wananchi katika kata hiyo walihama katika kipindi hicho cha ukame mkubwa zaidi, kuliko miaka yote.

"Anasema kwa mwaka 2019, kata nzima yenye vijiji vitano na jumla ya kaya 12 zimehama na kwenda katika mikoa mbalimbali, kwa ajili ya kutafuta maeneo ya kilimo, malisho ya mifugo na makazi.

"Kwa wastani kila kaya moja ina watu kuanzia sita na kati ya hao wanafunzi ni wanne, hivyo kuna zaidi ya watu 100 wamehama kwa mwaka huo na hao wameondoka na watoto wadongo ambao wangetakiwa kupatiwa huduma za afya hususani chanjo mbalimbali," anasema

**WANANCHI**

Dai la wananchi waliozungumza na Nipashe, ni kwamba kinachohitajika zaidi ni elimu kwa jamii ijue athari zinazoweza kutokea, endapo watashindwa kuwapatia haki ya msingi ya huduma za afya (chanjo) watoto wao.

Ngasa Jisenge, ni wanakijiji cha Mabambasi, anasisitiza haja ya elimu kutibu tatizo hilo, wananchi hawana uelewa kuhusiana na madhara yanayoweza kutokea, endapo mtoto atashindwa kupata chanjo zote.

"Elimu itolewe zaidi kwani kuhama siyo jambo baya, lakini mtoto akienda na taarifa zake muhimu, hata huko ambako anaenda ataendelea na huduma hizo hizo vizuri. Ni elimu tu inahitajika kwa wingi," anasema Jilala.

Aidha, dai lingine la wananchi hao wanataka kuwepo sheria ya kuwabana wanaohama, kuhakikisha wanawapatia watoto huduma zote zinazohitajika, hata kama watahama, bali liwepo hitaji lia kuwafuatilia.

"Elimu imekuwa ikitolewa, lakini wengi hawaelewi. Ni vyema serikali ikaweka sheria kali, watu wandelee kuhama lakini wahakikishe zile haki za msingi za mtoto zinaendelezwa na siyo kumpeleka porini kulima au kuchunga," anasema Masunga John.

**Serikali.**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwamanimba, Jilala Mahona, anasema elimu wanaitoa kila mara, lakini mazingira na hali ya hewa ya wilaya hiyo, ndiyo msukumo mkuu wa watu hao kuhama.

" Hata kama tatizo ni ukame, tunawaambia kutoa taarifa ni muhimu na watoto wawachukulie uhamisho, lakini wengi hawajali hilo, na sisi kuwafuatilia hatuna uwezo huo kwani kunahitaji gharama kubwa," anasema Jilala.

Ofisa Mtendaji wa Kata, Manota, anasema wamekuwa wakiwasiliana na viongozi wenzao kwenye mikoa wanakohamia, lakini tatizo limekuwa gharama ya kufuatilia.

Manota anasema, hivi karibuni wamefanikiwa kumrudisha mwanafunzi mmoja aliyetakiwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu, kwani wazazi wake walihama naye, baada ya kufanya mtihani.

" Tumefanikiwa kumrejesha kwa kushirikiana na viongozi wenzatu huko walikokuwa na ameanza shule. Tatizo ni kubwa, lakini kuweza kupamba nalo hapo kuna ugumu kidogo," anasema Manota.

# Kijue kitunguu maji na faida zake kwa afya yako



Bidhaa ya kitunguu, kizima na kilichokatwa. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

KITUNGUU maji ni aina ya mboga yenye harufu kali inayochangamsha mwili. Pia, ni kiungo ambacho kina virutubisho katika vyakula na kuvifanya viwe na ladha nzuri.

Nchi mashuhuri na maarufu inayolima kiungo hicho ni Misri na kusambaa zaidi duniani na nchini Tanzania, kinalimwa zaidi katika mikoa kama Morogoro, Iringa, Arusha kwenye rutuba nzuri ya kustawisha kiungo hicho.

Vinaelezwa kitaalamu ni aina ya mboga ya 'Yungiyungi na inatajwa kuthibitika kisayansi kuwa na manufaa makubwa sana katika afya ya mwanadamu.

Kiungo hicho kimekuwa kikitibu na kuponya maradhi mbalimbali kutokana na kuwa na madini ya salfa ambayo ni nzuri, hasa kwenye ini na husaidia kuponya kansa kwenye utumbo na kinywa, kutokana na kuwa na virutubisho vingi vya vitamini C.

Kitunguu maji kina kazi nyingi mwilini mwa binadamu, inatibu magonjwa ya kikohozi, vidonda vya tumbo na mifupa, ngozi koo, figo, tumbo na mkojo, kufunga hamu ya kula, hutia kiu na hulainisha tumboni.

Pia, ni chanzo cha madini mengi yanayopatikana katika kiungo hicho, ambayo ni umuhimu katika mwili wa binadamu.

Licha ya umuhimu huo, pia inamarisha afya ya moyo, kuzuia kansa, inakinga mwili dhidi ya vidonda vya tumbo na kuongeza joto la mwili, ikizuia vimelea vya magonjwa mbalimbali katika mwili wa binadamu.

Faida zake katika mwili wa binadamu ni pamoja na kuupa mwili nishati, kuongeza nguvu, huimarisha misuli ya mwili, kuongeza hamu ya kula, inalainisha tumbo na kuondoa tatizo la kukosa choo.

Pia, faida nyingine ya kitunguu ni kuwa kinatibu pumu, uvimbe wa pafu, saratani, majipu, mvilio wa damu, kufungua choo, kupunguza uzito na chunusi.

Kitunguu maji kinaweza kutengenezewa juisi kwa kukikatakata na kisha kukisaga kwa blenda kwa kuchanganya na maji ya kunywa mara unapojisikia vibaya hasa kwa watu ambao wanasumbuliwa na kifua mara kwa mara.

Pia, unaweza kuchanganya na asali na kunywa nayo ikakusaidia kwa kiasi kikubwa kutibu maumivu ya tumbo na uvimbe mwilini. Maji ya kitunguu kwa mujibu wa wataalamu wa tiba wanasema yanatibu matatizo ya macho.

Juisi yake inaua vijidudu vya kifua kikuu. Kuna tafiti za kisayansi zinazobainisha kuwa na mchango katika kuwa na uwezo wa kuua vijidudu vinavyosababisha maradhi ya kifua-kikuu(baada tu ya mgonjwa kunusa moshi wake)

Uso nao unanawiri pale kitunguu kuchomwa kinapoliwa huufanya uso kuwa mweupe, mn'gavu na unaonawiri.

Kingine, kinasaidia tatizo la kukosa haja kubwa, huku kikipikwa na kuliwa pamoja na samli, kusaidia kuongeza nguvu za kiume.

Upande wa kinamama, kitunguu kikitengenezwa supu pamoja na nyama, huongeza hamu ya tendo la ndoa kwa wanawake.

Kinasaidia kutibu homa ya manjano na kinavunja mawe tumboni na kutibu tatizo la hedhi kwa wanawake.

Ina msaada kwa wagonjwa wa kisukari, maradhi ya moyo, na kuimarisha mfumo wa mzunguko wa damu mwilini.

Ina sumu vyenye nguvu inayoua kaswende, kisonono.

***Ni kwa mujibu wa taarifa za afya mtandaoni. Jinsi kilimo chake kinavyoendeshwa, fuatilia makala kesho.***

AFYA

# Corona inavyozidi kuitesa dunia


- Italia vifo tishio, China nafuu
- Vifo; kinababa wako 70%
- Hatua katika utafiti chanjo
- Klorokwini ina nafasi kutibu
- Imezua mfumo mpya maisha




Wanunuzi wakiwa kwenye foleni nje ya maduka ya kisasa nchini Uingereza

**Na Jackson Paulo**

***Sehemu ya kwanza ya makala hii Alhamisi wiki iliyopita, iliainisha kwa kina picha halisi ya maradhi corona kwa undani, kwa mujibu wa ufafanuzi kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO). Ifuatayo ni sehemu ya pili, ikianisha hali yaliyo inayoendelea kuhusu ugonjwa huo, maambukizi na tiba yake, pia kasi ya maambukizi. Endelea.***




MAAMBUKIZI ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19, yamezidi kuenea kwa kasi duniani kote, huku idadi ya vifo nayo ikigoma kupungua.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linaesema kuwa bado linaendelea kufanya uangalizi wa karibu juu ya maendeleo ya ugonjwa wa COVID-19.

Waziri wa Afya wa Uingereza, Nadine Dorries, Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel, ni miongoni mwa waliogundulika kuwa na korona.

> **Hadi kufika Machi 20 shirika hilo lilisema idadi ya maambukizi yaliyothibitishwa yalikuwa watu 266,073, na idadi ya vifo11, 184.**

**Maambukizi,vifo**

Tangu kugundulika kwa virusi vya corona, idadi ya maambukizi na vifo imezidi kuongezeka siku hadi siku.

WHO inaeleza, hadi tarehe 20 Januari idadi ya maambukizi yaliyothibitishwa yalikuwa watu 282 na kwa wakati huo nchi nne pekee ndio zilikuwa zimethibitika kuwa na waathirika wa corona. Hizo ni nchi za China (278), Thailand (2), Japan na Korea, kila moja ilikuwa na mgonjwa mmoja.

Hadi kufika Machi 20 shirika hilo lilisema idadi ya maambukizi yaliyothibitishwa yalikuwa watu 266,073, na idadi ya vifo11, 184. Hapo kukiwepo jumla ya maeneo 185 yenye maambukizi.

Katika kipindi cha siku12 zilizopita, tayari inaelezwa idadi ya vifo vimeongezeka kutoka watu 4, 012 hadi kufikia 11,184.

**Wanaume hatarini**

Katika hali inayowashangaza wanasayansi, idadi ya waliofariki dunia kutokana na virusi vya corona imeonekana kuwa na tofauti mkubwa ki jinsia.

Nchini Italia ambayo ndipo palipothibitishwa vifo vingi zaidi duniani hadi 20 Machi, kati ya vifo vyote vilivyotokana na Covid-19, wanaume walikuwa ni asilimia 70, huku wanawake wakiwa asilimia 30.

Hata hivyo, takwimu zimeonyesha kuwa wanaume wamekuwa kwenye uwezekano mkubwa zaidi ya kupata maambukizi ambazo kati ya walioambukizwa nchini humo 60 ni wanaume.

Nchini China ambapo janga hili linasadikika kuanzia utafiti umeonyesha kwamba, karibu theluthi mbili ya wagonjwa waliokwishafariki kwa Covid-19 walikuwa wanaume.

Watafiti hao wanaeleza, pengine takwimu zimekuwa hivyo, kutokana na sababu kuwa wanaume ndio wanaoshiriki zaidi katika uvutaji sigara na unywaji pombe, japokuwa hii imekuwa ni sababu ya kitamaduni zaidi ambayo inaweza kuwa tofauti katika nchi zingine.

Wanasayansi wanasema hawajajua kwanini wanawake wanaonekanakuwa katika hatari ndogo zaidi ya kufariki kutokana na Covid-19, lakini wanaeleza kuwa kwa asili wanawake wana kinga ya mwili iliyo imara zaidi, kuliko wanaume na wana uwezekano mdogo kuwa na hali ya matatizo ya kiafya ya muda mrefu.

WHO na wanasayansi wa China, walifafanua mwanzoni mwa Machi kwamba, kiwango cha uwezekano wa kufariki baada ya kupata virusi vya corona, ilikuwa asilimia 1.7 kwa wanawake, ikilinganishwa na asilimia 2.8 kwa wanaume.

Sababu zinazoleta tofauti kati ya wanawake na wanaume bado hazijajulikana wazi. Wataalamu wanashauri kuwa, wanaume wanapaswa kuwa waangalifu zaidi, katika kujiepusha na virusi vya corona.

**Chanjo ya corona**

Tafiti mbalimbali zinaendelea kuhusu chanjo ya virusi vya corona katika mataifa kadhaa. Ka-

INAENDELEA UK.19

AFYA

# Corona inavyozidi kuitesa dunia

INATOKA UK.18



Mwanamfalme wa Uingereza Prince Charles, naye ametangaza kupatwa na corona. **PICHA: MTANDAO.**

tika nchi ya Marekani kumekuwa na matumaini juu ya uwezekano wa kupata chanjo, ambayo jaribio limeshafanyika kwa binadamu.

Nchini Uingereza, majaribio ya chanjo yanatarajiwa kufanyika kwa wanyama wiki hii na majaribio kwa binadamu kuanza mwezi Aprili. Hata hivyo, wanasayansi wanasema chanjo hiyo haitaweza kupatikana na kutumika ndani ya muda mfupi ujao.

Hivyo, pengine angalau mwaka ujao ndio chanjo inaweza kuanza kutumika rasmi. Yote hiyo ni kutokana na utaratibu unaopaswa kufuatwa kuanzia ugunduzi, hadi matumizi ya dawa yoyote mpya.

Ugunduzi chanjo huhusisha awamu tatu; awamu ya kwanza ni kuangalia iwapo chanjo hiyo ni salama kwa binadamu kwa kutumia wanyama na idadi ndogo ya watu, ili kupima iwapo inatoa majibu sahihi kuamsha kinga ya mwili.

"Hata kama mambo yatafanyika kwa haraka, hatua hii ya awali itachukua miezi miwili hadi mitatu kukamilika" anasema Prof Robin Shattock, wa Chuo cha Imperial London.

Hatua inayofuata ni kuitoa chanjo hiyo kwa kiwango kikubwa zaidi na kuanza kuangalia kama inaweza kuzuia maambukizi katika jamii. Hapa unahitajika takwimu zenye kuonyesha namna gani, inafanya kazi kabla ya kupata leseni ya kuiuza kama bidhaa.

Katika awamu ya tatu, majaribio makubwa zaidi hufanyika kabla ya kuidhinishwa rasmi. Hata hivyo, katika hali za dharura, chanjo za majaribio hutolewa mapema kwa wafanyakazi waliopo sekta muhimu.

**Klorokwini inatibu**

Huku tafiti juu ya chanjo dhidi ya virusi vya corona zikiendelea, Rais wa Marekani Donald Trump, ametangaza kuwa nchi yake imethibitisha kuwa dawa iliyowahi kutumika kutibu malaria aina ya Chloroquine inafanya kazi vizuri katika kukabiliana na virusi vya corona. Rais Trump anasema, mamlaka ya chakula na dawa (FDA) imethibitisha ufanisi wa dawa hiyo dhidi ya corona.

"Tutaweza kuanza kutengeneza dawa hiyo mara moja. FDA imefanya vizuri sana na sasa wameshapitia mchakato wa kutafuta idhini na imeshapitishwa" anasema Rais Trump.

Walakini, FDA imeweka wazi kuwa bado chloroquine haijapitishwa kwa ajili ya kutibu wale walioambukizwa virusi vya corona.

"Hakuna matibabu wala dawa zilizokubaliwa na FDA za kutibu, kuponya au kuzuia Covid-19," anasema FDA, imeongeza kuwa tafiti bado zinaendelea, ili kuona kama chlokwini inaweza kutumika katika matibabu ya Covid-19.

Mamlaka hiyo imesema kuwa imeelekezwa na Rais Trump, kuanzisha kliniki kubwa ya kufanya majaribio ya dawa hiyo.

> **"Hakuna matibabu wala dawa zilizokubaliwa na FDA za kutibu, kuponya au kuzuia Covid-19," anasema FDA, imeongeza kuwa tafiti bado zinaendelea, ili kuona kama chlokwini inaweza kutumika katika matibabu ya Covid-19.**

Aidha, katika maelezo mafupi baadaye, Trump alisema klorokwini imepitishwa kwa "matumizi ya huruma".

Ni jambo linakuwa na maana kwamba, daktari anaweza kumpa mgonjwa dawa ambayo bado haijakamilika kuidhinishwa na serikali, ikiwa mgonjwa yupo katika hatari ya kupoteza maisha.

Madaktari wana uwezo wa kutoa klorokwini katika hali kama hiyo, kwani ni dawa iliyokwishasajiliwa.

**Italia kinara**

Hali ya vifo na maambukizi imebadilika ghafla huku Italia ikiwa mstari wa mbele kwa idadi ya vifo vya Covid-19. Usiku wa kuamkia 21 Machi 21, nchi hiyo iliyo na idadi ya watu milioni 60 iliripoti vifo vipya watu 800 huku China yenye watu bilioni 1.4 ina vifo vipya vivane kwa mujibu wa WHO.

Taarifa kutoka Chuo Kikuu cha Johns Hopkins cha Marekani, zinaeleza hadi kufikia Machi 22 kulikuwapo vifo 4,825 amabayo ni sawa na asilimia 37.1 ya vifo vyote13,000 vinavyokadiriwa kutokea duniani kote.

China kwa sasa imeanza kuwa na ahueni ya corona, kwa idadi wagonjwa kushuka hadi kufika wanane Machi 20.

Kitaalamu, ni kiashiria kwamba, imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kudhibiti janga la corona.

**Maisha yabadilika**

Mara baada ya kasi ya virusi vya corona kuongezeka, nchi zimeanza kuchukua hatua kadhaa. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa hadi sasa ni pamoja na kufunga mipaka, kusimamisha shughuli zote zenye mkusanyiko ikiwamo mashindano ya michezo mbalimbali, matamasha na marufuku ya watu kutoka nje ya majumba yao.

Katika nchi za Ulaya na Marekani, wananchi wamekuwa wakishauriwa kubaki majumbani kujiepusha na maambukizi ya virusi vya corona.

Ni hali inayosababisha misongamano mikubwa katika maduka ya kisasa, huku kila mtu akitaka kujipatia mahitaji muhimu akiwa nyumbani, hiyo ikishuhudiwa katika nchi kama Uingereza na Marekani, foleni kuanzia nje ya maduka.

Nchini Tanzania (Bara), mara baada ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee Ummy Mwalimu, alianza kwa kutahadharisha haja ya kusungatia kanuni muhimu za kujihami.

Baada ya kuthibitika kuwepo maradhi hayo, serikali kupitia Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ilitangaza kufungwa kwa shule zote kuanzia za awali hadi vyuo vikuu kwa muda wa siku 30.

Hadi sasa kuna marufuku ya mikusanyiko na kuwataka wananchi kuchukua tahadhari kila mara. Baadhi ya wananchi nao wameonekana wakivalia barakoa 'mask' katika maeneo mbalimbali japokuwa hazishauriwi kuvaliwa na kila mtu, kila wakati.

Wanunuzi wakiwa kwenye foleni nje ya Supermarket nchini Uingereza

**Dalili za corona**

Baadhi ya walioambukizwa virusi vya corona hawaonyeshi dalili. Hata hivyo, pale virusi vinaposababisha dalili za kawaida huwa ni pamoja na homa ya kiwango cha kawaida, maumivu ya mwili, kukohoa, kutoka kamasi puani na maumivu sehemu ya koo.

Hata hivyo, virusi vinaposababisha dalili za kina ni pamoja na homa kali, kikohozil, na kubanwa pumzi ambazo mara nyingi huashiria homa ya mapafu.

**Jinsi ya kujikinga**

Osha mikono yako mara kwa mara kwa sabuni na maji au 'sanitizer.'

Epuka kukaribiana sana na mtu (angalau mita moja).

Epuka kugusa macho yako, pua au mdomo.

Kaa nyumbani ikiwa unahisi wewe ni mgonjwa.

Funika kinywa wakati wa kukohoa au kupiga chafya (kwa kutumia kiwiko)au piga chafya kutumia tishu, kisha utupe tishu hizo kwenye chombo cha taka.

Safisha na weka dawa ya kuua vijidudu vitu au sehemu zinazoguswa mara kwa mara.

*Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa rasmi za kimataifa za afya, hadi juzi. Mwandishi anapatikana kwa baruapepe: jacpole@gmail.com

AFYA

# Mama wa mwenye ualbino asimulia majaribu ya mkunga

## • Asifu ushujaa wa mume ulivyombadili

**Na Romana Mallya**

STELLA Bulinda ni mama wa watoto wawili, wenye ualbino. Binafsi anaanza kwa shukurani kupitia imani ya imani ya Mungu, akieleza anawapenda sana wanawe.

Mama huyo, mwaka 2017 alipojifungua mtoto wa kwanza wa kike, alitekwa na fikra za kukatishwa tamaa, kupitia kauli ya muuguzi aliyemhudumia baada tu ya kujifungua .

Ilikuwaje? Stella, mkazi wa Bunju jijini Dar es Salaam, aliyeolewa na mume anayemtaja kwa jina la Bulinda, alisimulia hayo hivi karibuni, katika mafunzo ya wanawake walio na watoto wenye ualbino, kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Ilikuwa Jumamosi ya Machi 7 ikiwa ni siku moja kabla ya kilele cha maadhimisho hayo, wanawake wenye watoto walio na vinasaba hivyo, walikutana katika viwanja wa Shirika la Kimataifa la Under The Same Sun (UTSS) jijini Dar es salaam, kujadili siku yao.

Anasema, mada kuu haikulenga zaidi kuzamakatika changamoto zao, ingawa kauli ya Stella iliangukia msingi wa 'kila penye mafanikio, matatizo hayakosekani' au kinyume chake.




Stella Bulinda, mkazi wa Bunju jijini Dar es Salaam, alipozungumza mafunzoni. **PICHA: ROMANA MALLYA.**

### ILIKUWAJE?

Stella anasimulia mwaka 2017 alipojifungua mtoto wa kwanza baada ya kuolewa, muuguzi alimtamikia kauli iliyobeba maudhui anayotafsiri ama ni kejeli na kashfa, kupitia swali: "Mtoto wako ni huyu umejifungua wa kike, kwenu kuna hawa?."

Mzazi huyo anaeleza mapokeo ya hisia yake, akisema: "Kauli hii ilinipa shauku kutaka kumuona mtoto niliyejifungua ni wa aina gani na kwa haraka akilini mwangu nilijiuliza nimejifungua nini? kwa nini kauli hiyo ya muuguzi?

"Haraka nilimchukua mtoto, ndipo nilipobaini nimepata mtoto mwenye ualbino, ingawa sikutarajia kujifungua mtoto mwenye ualbino. Lakini kama ilivyo kwa mama yoyote duniani akijifungua, kauli kama ile aliyoitoa muuguzi ilinikatisha tamaa na kunivunja moyo.

"Kwa kweli kama mzazi na kitu ambacho sikutegemea, ilinishtua sana na niliumia sana kwa muda ule.Nilimchukua mtoto wangu, nikambeba na muuguzi alipoondoka nilichukua simu na kumpigia mume wangu ambaye wakati ule alikuwa nje."

Stella anaendelea: "Kama ilivyo kwa mama yoyote duniani anapojifungua huwa na shauku la kumjulisha mzazi mwenza, ndivyo nilivyofanya. Nilimpigia simu mume wangu kumpa habari njema kuwa tumepata mtoto wa kike."

> "Huwezi amini, wakati naondoka wodini nikiwa na mtoto na mume wangu, nakumbuka ilikuwa siku ya pili baada ya kujifungua. Nilijiona ni mwanamke aliyebahatika kupata mtoto wa pekee.

Stella anasimulia kuwa mume wake alipopokea simu, alimtamkia:"Tumepata mtoto wa kike kama ulivyokuwa unahitaji na mtoto wetu ana ualbino."

Mwanamke huyo anasema, tofauti na matarajio yake, mumewe alikuwa wa kwanza kumfanya ajione ni mwanamke pekee na mtoto waliompata ni baraka kutoka kwa Mungu.

Anaendeea kusimulia mkasa wa historia hiyo, akinukuu marejeo ya mume:"Hakuna shida mke wangu mpenzi, kila kitu ni mpango wa Mungu. Kwa hiyo, usimpangie Mungu, shukuru Mungu umejifungua salama na mpo salama na mtoto na umejifungua mtoto ambaye ni 'special' (wa kipekee)."

Stella ambaye ni mfanyabiashara, anasema ni kauli iliyompa faraja iliyomfungulia ukurasa mpya wa kiimani, ajione amebarikiwa, tofauti na wenzake wodini.

"Huwezi amini, wakati naondoka wodini nikiwa na mtoto na mume wangu, nakumbuka ilikuwa siku ya pili baada ya kujifungua. Nilijiona ni mwanamke aliyebahatika kupata mtoto wa pekee.

"Wakati ninaondoka wodini, wanawake wenzangu walikuwa wananishangaa, wauguzi wanishangaa, sijui walitegemea tofauti. Nilijawa amani moyoni na uso wenye tabasamu. Hii yote ilitokana na maneno ya mume aliyonieleza, nilipompa habari njema ya kujifungua salama," anasema.

Stella anasema baada ya kufika nyumbani, mtu wa pili ambaye alimtia moyo ni baba wa kiroho (kiongozi wa kiimani ), aliyewaita na mume wake azungumze nao.

"Nakumbuka maneno yake aliniambia Stella, mshukuru Mungu umetoka salama. Halafu mtoto ni zawadi kutoka kwa Mungu na Mungu amekupa kwa sababu anajua unaweza kumlea na kumtunza. Wewe ni wa pekee amekupa mtoto wa pekee.

Anakiri kauli hiyo ya pili, iliwanya wote wawili kutembea 'kifua mbele' na kuzidisha upendo zaidi kwa mtoto wao, huku wakati wote wakimuombea akue na kufikia kutimiza ndoto zake.

Stella anasimulia kwambna, wakati akiendelea na malezi ya mtoto wake wa kwanza, mwaka uliofuata 2018, alibarikiwa kujifungua mtoto wa pili wa kiume, naye alikuwa mwenye ualbino.

"Nakumbuka wakati najifungua mume wangu alikuwa safarini. Nilimpigia simu kumtaarifu kuwa nimejifungua salama na mtoto tuliyempata ni wa kiume na amefanana na mtoto wetu wa kwanza.

" Kama kawaida ya mume wangu, alipokea taarifa hii kama ilivyokuwa ya mtoto wetu wa kwanza," anasema.

### JAMII INAVYOMCHUKULIA

Stella anasema, kwa kawaida ni vugumu majirani kuzungumza chochote, lakini siyo wote walioelewa hali hiyo. Aanaendelea:"Kukwambia moja kwa moja mpaka sasa sijawaona watu wa namna hii, ila kuna baadhi ya watu naona wanapungua katika maisha yangu.

"Ila kupungua kwao katika maisha yangu, haikunikatisha tamaa, kwa sababu kuna watu wananishika na kuwa bega kwa bega name. Wa kwanza ni mume wangu mpenzi tumeshikana pamoja.

"Mwingine ni mama yangu na watumishi ambao walitumwa na Mungu kwa ajili ya familia yangu wamekuwa nasi bega kwa bega."

### NENO LAKE

Stella ana wito kwa jamii kuwa wanapaswa kuwa na uelewea mzuri, pindi wanapojifungua mtoto mwenye ualbino, kwani daima hakuna ubaya, bali ina upekee kama iivyokuwa kwake.

Pia, anatahadharisha tabia ya wanaume wanaokimbia familia mara wapatapo mtoto mwenye ualbino, hata marukio ya mwanamke kumtelekeza mtoto.

"Mshukuru Mungu na umwambie 'ninakuangalia wewe kwa sababu wewe ndiye uliyenipa mtoto huyu mwenye ualbino na kwa sababu unajua ninao uwezo wa kumlea, kumlinda na kufanikisha ndoto zake," anasema, akisisitiza mzazi kumuwajibikia kila mtoto.

Moja ya eneo muhimu anazozitaja ni kuwawezesha watoto kujitambua, wapewe ulinzi na haki yao ya kupata elimu na kuelimika, ili wawe na tafsiri sahihi ya ualbino na maisha yao .

"Tukifanya hivyo hatutaongelea mauaji, hatutaongelea unyanyapaa, hatutaongelea baba au mama kukimbia familia, tutalisaidia kundi hili kutembea zaidi kifua mbele mijini na vijijini, iwe mchana au usiku," anasema.

"Binafsi katika mafunzo haya, nimejifunza zaidi upendo na ushirikiano siyo tu kwa watoto wenye ualbino, bali pia kwa jamii kwa ujumla. Ninalishukuru Shirika la Under The Same Sun kwa kuandaa mafunzo haya ambayo naamini tulivyokuja ni tofauti na tutakavyoondoka," anasema.





Wahandisi wa Wakala wa Barabara nchini (Tanroads), Mkoa wa Mbeya, wakishirikiana na mkandarasi anayejenga barabara ya Chunya-Makongorosi mkoani Mbeya jana, kutengeneza kwa dharura daraja la Mto Lupa, ambalo lilisombwa na maji na kusababisha mawasiliano kukatika. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wawili wafa ajali ya basi na bajaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA MJINI

WATU wawili wamepoteza maisha katika ajali ya barabarani iliyohusisha basi la abiria linalofanya safari zake kati ya Mbeya na Ifakara mkoani Morogoro lililogongana uso kwa uso na bajaji eneo la Ilomba jijini Mbeya.

Akizungumza na wandishi wa habari jijini hapa jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alilitaja gari lililohusika kwenye ajali hiyo kuwa ni lenye namba za usajili T 413 AVU, mali ya Kampuni ya Rahabu ambalo liligongana na bajaji yenye namba za usajili MC 230 BGT aina ya TVS.

Alisema ajali hiyo ilitokea juzi saa 12:15 asubuhi wakati mabasi yalipokuwa yanaanza safari zake kutoka jijini Mbeya kwenda maeneo mbalimbali nchini.

Aliwataja waliofariki dunia kwenye ajali hiyo kuwa ni dereva wa bajaji ambaye jina lake bado halijafahamika pamoja na abiria wake, Ester Mbonje (35), mkazi wa Ilemi jijini Mbeya.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa basi kuendesha gari bila kuwa makini kwa kutaka kulipita gari lingine bila kuangalia mbele na hivyo kukutana na bajaji uso kwa uso na kupelekea bajaji hiyo kupinduka. "Baada ya kugongana, bajaji ilipinduka na kuwasababishia majeraha waliokuwa ndani yake, wawili hao walifariki dunia wakati wanaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya," alisema.

Kamanda Matei alisema kuwa baada ya ajali hiyo kutokea, dereva wa basi, Ayoub Mwandwanga (36), ambaye ni mkazi wa Ilomba jijini Mbeya, alikamatwa na anaendelea kushikiliwa na polisi wakati akisubiria hatua zaidi za kisheria.

Alisema Jeshi la Polisi linaichukulia ajali hiyo kuwa ni ya makusudi kutokana na namna ambavyo dereva wa basi hilo alivyofanya kile alichokiita uzembe.

Aliwataka madereva wa vyombo vya moto mkoani humo kuwa makini kwa kufuata sheria na taratibu za usalama barabarani ili kuepuka kusababisha ajali ambazo hazina ulazima.

Kamanda Matei alisema miili ya marehemu imehifadhiwa kwenye hospitali hiyo ya kanda, akiwataka wananchi kwenda kuutambua mwili wa dereva wa bajaji.

# Mganga Mkuu atoa hadhari ya corona

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA MJINI

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, amewataka wananchi mkoani humo kuendelea kufuata taratibu zinazoelekezwa na wataalamu wa afya kuhusu namna ya kujikinga na maambukizo ya virusi hatari vya corona.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, Dk. Manyatta alisema mkoa huo hauna mgonjwa wa virusi hivyo, lakini wananchi wanatakiwa kuendelea kufuata masharti ili visiingie.

Alisema moja kati ya masharti ambayo wanatakiwa kuyazingatia ni pamoja na kuhakikisha wananawa mikono kwa kutumia maji safi yanayotiririka na sabuni na kutumia vitakasa mikono.

Aliwasisitiza wananchi kuacha kusalimiana mikononi na kukumbatiana na badala yake watumie njia nyingine ikiwamo kusalimiana kwa kugonga miguu au kwa maneno bila kugusana.

"Hatuna mgonjwa hata mmoja katika mkoa wetu, lakini ugonjwa huu tayari upo nchini na takwimu zinaonyesha mpaka sasa ni wagonjwa 12, hivyo ni lazima kila mmoja wetu achukuwe tahadhari ili tusiathirike na ugonjwa huu," alisihi.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo kuepuka kusafiri bila sababu hasa kuelekea kwenye mikoa ambayo tayari ina wagonjwa wa corona kwa kuwa wanaweza wakapata ugonjwa huo.

Aliwataka wananchi kutoa taarifa kwenye mamlaka za serikali kuhusu mtu yeyote ambaye watamwona kuwa na dalili za ugonjwa huo hatari ili taratibu za kuhudumiwa zichukuliwe mapema.

Alikumbusha kuwa tayari serikali imeelekeza kila taasisi ya umma kuandaa maji safi na sabuni kwa ajili ya wageni kunawa kabla hawajaingia kwenye ofisi zao ili kuepuka ugonjwa huo kusambaa.

# 'Mitandao ya kijamii itumike kutoa elimu kuikabili corona'

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA MJINI

WADAU wamesisitiza kutumia mitandao ya kijamii, ikiwamo Facebook na WhatsApp, kutoa elimu ya kujikinga na maambukizo ya virusi corona nchini.

Mkurugenzi wa shirika lisilokuwa la kiserikali linalotoa elimu kwa vijana kupitia michezo la YEs-Tz, Kenneth Simbaya, aliiambia Nipashe jana kuwa kuna haja mitandao hiyo itumike ipasavyo kusambaza elimu ya kujikinga na virusi hivyo hatari.

Alisema njia moja wapo ya kukabiliana na maambukizo ya ugonjwa huo ni kutumia mitandao ya kijamii kama vile Facebook ambao una watumiaji wengi, kutoa elimu. "Ni jukumu letu sote kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona kila mmoja kwa nafasi yake achukue tahadhari, mimi na shirika langu tutajikita kutoa elimu kupitia Facebook na imani watu wengi watasoma," alisema.

Aliongeza kuwa shirika hilo lina lengo la kuwafikia vijana wengi mkoani Mbeya na katika kipindi hiki linawapa elimu ya uhusiano ili kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

Mratibu wa shirika hilo, Navina Mutabazi, alisema bado elimu inaendelea kuwafikia vijana kwa njia mbalimbali, ikiwamo kupiga simu kwa kushirikiana na wataalamu wa afya kwa kutumia mitandao ya kijamii.

"Taasisi yetu inaendelea kuwafikia vijana zaidi kuhakikisha elimu ya afya ya uzazi, masuala ya makuzi, wanapata kutoka kwa waelimishaji rika waliopo katika maeneo mbalimbali, elimu yetu inaanzia kwa vijana waliopo nje na waliopo shule," alisema.

Baadhi ya wakazi wa Jiji la Mbeya walipongeza hatua hiyo ya kutoa elimu ya maambukizo ya corona kwa kutumia mitandao ya kijamii, wakiamini itawafikia wengi.

Mmoja wa wakazi hao, Jesca Mwaipaja, alisema ni miongoni mwa wananchi watakaokuwa wanatembelea mtandao wa Facebook mara kwa mara ili kupata elimu ya kujikinga na virusi hivyo vinavyoisumbua dunia kwa





# Mchakato kuchagua wa kidato cha tano waanza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imesema uchaguzi wa wanafunzi kujiunga na kidato cha tano na vyuo vya ufundi, utafanyika baada ya kubadili tahasusi au kozi walizochagua awali ili wasome wanachokitaka.

Uchaguzi huo utawahusu wanafunzi 135,301 wenye ufaulu kuanzia daraja la kwanza hadi la tatu ambao walihitimu kidato cha nne mwaka 2019.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tamisemi, Selemani Jafo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ubadilishaji wa tahasusi na kozi utakaofanyika kwa njia ya mtandao kuanzia Machi 25 hadi Aprili 19, mwaka huu.

Alisema utoaji wa fursa ya kufanya mabadiliko kwenye tahasusi na kozi umetokana na baadhi ya wanafunzi kutojaza kwa uhakika tahasusi zao kwa kutokuwa na uhakika wa ufaulu katika masomo yao.

"Uzoefu umetuonesha miaka ya nyuma wanafunzi walikuwa wakifanya mitihani yao na kujaza fomu za kuchagua tahasusi na kozi (Selform) na baada ya matokeo kutoka wanafunzi inabidi aende kusoma tahasusi aliyoichagua shuleni, imesababisha wengine kupata matokeo tofauti au kubadilisha malengo ya anachotaka kusomea," alisema.

Alisema fursa hiyo itasaidia wanafunzi kurekebisha machaguo yao kulingana na ufaulu walioupata kwenye matokeo ya Kidato cha nne 2019 yaliyotangazwa na Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA).

Alibainisha kuwa wanafunzi hao watakuwa na uwezo wa kubadili machaguo au kuchagua kutoka kidato cha tano kwenda Chuo au Chuo kwenda kidato cha tano.

Jafo alifafanua kuwa hatua hiyo inatoa mwanya kwa mwanafunzi kusoma fani itakayomwandaa kuwa na utaalam fulani katika maisha yake ya baadaye kwa namna ambayo anatamani yeye mwenyewe au kwa kushauriwa na wazazi au walezi wake.

"Mabadiliko haya yanafanyika kupitia mtandao kwenye anuani selform.tamisemi.go.tz , ikitokea hadi baada ya Aprili 19, mwaka 2020 mwanafunzi hajabadili Tahasusi maana yake chaguo lake la awali ndo hilo hilo hatutaki kuona malalamiko yeyote," alisema.

Kadhalika, alisema ili mhitimu aweze kuingia kwenye mfumo itabidi kutumia namba ya mtihani wa kuhitimu kidato cha nne mwaka 2019, na taarifa nyingine atakazoulizwa mfumo.

Kwa mujibu wa Jafo, baada ya zoezi hilo Ofisi yake haitapokea maombi ya kubadili tahasusi na ambaye hatabadili taarifa zake kwa kipindi husika.

"Huu ni mwaka wa pili kutumia mfumo huu, na timu yetu imejiandaa vizuri kwa tatizo lolote litakalojitokeza, watu wa Tehama wamejipanga vizuri," alisema.



Wananchi wakinawa maji yasiyo salama yanayotiririka barabarani katika eneo la Ipagala, jijini Dodoma jana, kitendo ambacho ni hatari kwa afya zao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Walio hatarini kupata TB watajwa

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa wazee, watoto na watu wenye magonjwa sugu wapo hatarini kupata maambukizi ya ugonjwa wa kifua kikuu kutokana na miili yao kuwa na kinga dhaifu.

Hayo yalielezwa jana na Mratibu wa kifua kikuu na ukoma jiji la Dodoma, Dk. Peres Lukango, alipokuwa akizungumza na Nipashe, ikiwa ni siku moja baada ya maadhimisho ya siku ya kupambana na kifua kikuu Duniani ambayo hudhimishwa Machi 24.

Alifafanua kuwa makundi hayo yanahatari kubwa ya kupata ugonjwa huo, kutokana na kinga ya mwili kushuka hasa kwa wazee.

"Kwa upande wa watoto katika uchanga wao mfumo wa kinga haujakomaa unaweza kusababisha kupata kifua kikuu," alisema Dk. Lukango.

Aidha, Dk. Lukango alisema jiji hilo lina mikakati mbalimbali ya kuwatafuta, kuwafikia, kuwachunguza watu wenye maambukizi ya ugonjwa huo na endapo ikithibitika wameambukizwa, wanashauriwa kuwahi kupata huduma ya matibabu.

"Kipindi cha nyuma tulikuwa tunafanya kazi hii kwa kusubiri wagonjwa waje kwenye vituo vya afya, lakini kama mtu yuko nyumbani kwake anakohoa leo, kesho, kesho kutwa akaenda duka la dawa, akanunua dawa, akaenda kwa waganga, lakini imefika mahali sasa wanatoka huko walipo wanakuja vituo vya afya kwa ajili ya kupata ushauri wa kitalaamu," alisema Dk. Lukango.

Sambamba na hilo, alisema wamekuwa wakizunguka katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ugonjwa huo.

Naye, Mhudumu wa afya ngazi ya jamii, Rose Lema, alisema wamekuwa wakiwafuatilia wagonjwa ambao wameanza tiba ili wasiache na kuhudhuria kliniki inavyotakiwa kwa kuwa wakiacha dawa watakuwa na TB sugu.

# Kinamama, vijana kupewa mil. 207/-

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kongwa imetenga zaidi ya Sh. milioni 206.9 katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya mikopo ya makundi vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Hayo yalielezwa na Mkurungenzi wa Halmashauri hiyo, Dk. Omari Mkulo, wakati alipozungumza na Nipashe kuhusu asilimia 10 ya mapato ya ndani inayotolewa kwa ajili ya makundi hayo.

Dk. Mkulo alisema halmashauri hiyo imetenga kiasi hicho ambacho ni fedha ya mapato yake ya ndani ikiwa ni asilimia 10 ya kwa ajili ya mikopo kwa makundi hayo.

Alisema wameendelea kutenga fedha hizo ili kuwasaidia vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kulingana sheria ya kuzitaka halmashauri zote kutenga fedha hiyo.

Alibanisha kuwa katika mwaka wa fedha wa 2019/20 unaoishia juni mwaka huu halmashauri hiyo ilitenga bajeti ya Sh. milioni 113.7 ambapo vikundi 44 vilikopeshwa.

Alisema katika bajeti hiyo ya mwaka huo ufafanuzi wa mikopo ulikuwa kwa kundi la vijana walipata asilimia 4 wanawake walipata asilimia 4 na kundi la walemavu walipata asilimia 2 .

Dk. Mkulo alisema mwitikio wa makundi hayo kujitokeza kuomba mikopo umekuwa mkubwa kutoka na wananchi kuelimishwa kuhusu haki yao ya kupata mikopo hiyo kisheria.

Hata hivyo alisema mwitikio kwa kundi la walemavu umekuwa mdogo kutokana na kutopata elimu ya mikopo iliyotengwa kwa ajili yao.

Kwa upande wake, Kaimu Ofisa Maendeleo Wilaya ya Kongwa, Faraja Kasuwi, alisema idara hiyo inaendelea kutoa elimu kwenye mikutano na nyumba za ibada kuhusu fedha hizo ili wananchi watumie fursa hiyo.

Kasuwi alisema mwaka huu wanakusudia kuwafikia makundi hayo kwa kufanya mikutano kila kata kuwahamsisha kuunda vikundi ili kupata urahisi wa kupata mikopo hiyo.

Aidha, aliwashauri wananchi kujiunga katika vikundi na kuibua miradi yenye tija na kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha ili kujikwamua kiuchumi.



# Zaidi ya madawati 4,000 kusambazwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya kitaifa ya madawati Zanzibar katika shule za msingi na sekondari inatarajia kuanza kusambaza madawati katika shule za Unguja na Pemba, 4,545 ambayo yamewasili nchini.

Mwenyekiti wa kamati ya kitaifa ya madawati kwa shule za Unguja na Pemba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba na Tawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari na kutembelea madawati yaliyowasili nchini yakiwa katika hatua za matayarisho ya kuunganishwa.

Alisema kamati ya kitaifa ya madawati imeundwa kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira mazuri na sio kukaa sakafuni.

Alisema juhudi kubwa zimefanywa kulipatia ufumbuzi tatizo la uhaba wa madawati nchini ikiwamo kukusanya michango kupitia njia za harambee na baadhi ya wahisani na wafanyabiashara kuchangia.

"Tatizo la uhaba wa madawati hivi karibuni tutalipatia ufumbuzi wake tayari tunayo madawati 4,545 ikiwamo viti na meza ambavyo tutasambaza kwa shule za Unguja na Pemba ili kukabiliana na uhaba uliopo kwa sasa," alisema.

Mkurugenzi wa Sera na Utafiti wa Wizara ya Elimu, Mafunzo ya Amali, Khalid Masoud alisema, jumla ya kontena tisa zimewasili nchini na zingine 13 zinasubiriwa.

Alisema wanafunzi 13,615 watafaidika na madawati hayo ambayo mahitaji yake makubwa yapo kwa upande wa shule za maandalizi na msingi.

"Matarajio yetu makubwa kwamba madawati haya yatasaidia kukabiliana na uhaba uliopo ambao zaidi kwa shule za maandalizi pamoja na msingi Unguja na Pemba," alisema.

Naye Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohamed Said, alisema tatizo la uhaba wa madawati ni kubwa zinahitajika juhudi kukabiliana na tatizo hilo.

Alisema kuongezeka kwa shule za msingi na sekondari Unguja na Pemba kumeibua tatizo la uhaba wa madawati ikiwamo viti na meza.

"Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imefurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na kamati ya kitaifa ya kukabiliana na tatizo la uhaba wa madawati nchini na juhudi zake tunaziona," alisema.

Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, aliunda kamati ya kitaifa kukabiliana na madawati kwa shule za Unguja na Pemba baada ya tatizo hilo kujitokeza huku wanafunzi wengi wa shule za maandalizi na msingi wakisoma chini ya sakafu.

# Z'bar yajizatiti kusimamia miradi ya maendeleo yake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Balozi Muhamed Ramia amesema licha ya uchumi kushuka kutokana na uwapo wa maradhi ya corona duniani, Serikali ya Zanzibar itahakikisha inaendelea kusimamia miradi ya kimaendeleo iliyoanzishwa ili imalizike kwa wakati.

Alisema miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa nyumba za mkaazi zilizopo mtaa wa Kwahani, jengo la Mahakama Kuu Tunguu, jengo jipya la abiria uwanja wa ndege na ujenzi wa mitaro ya kupitishia maji ya mvua.

Alisema hayo alitopafanya ziara kwenye miradi hiyo ikiwamo wa nyumba za Kwahani na jengo la Mahakama Kuu Tunguu.

Alisema, mpaka sasa hakuna changamoto yoyote inayokwamisha kuendelea na ujenzi wa miradi hiyo na fedha zipo.

Vile vile, aliwatoa hofu wasimamizi wa miradi na kuwataka kuendelea na kazi ya ujenzi wa miradi hiyo kama ilivyopangwa.

"Kuwapo kwa maradhi ya corona isiwe sababu na kukwamisha miradi hii, endeleeni na kazi kama kawaida na pale tutakapoona kuna changamoto basi hatutasita kutoa taarifa," alisema.

Balozi Ramia alisema, dunia mzima hali ya kiuchumi sio nzuri kutokana na kuwapo kwa ugonjwa huo na kuathirika kiafya na kiuchumi.

Alisema serikali inaendelea kufanya tathmini ya kina ili kujua kwa kiasi gani nchi imeathirika kiuchumi kutokana na kuwapo kwa ugonjwa huo.

Naye, Mshauri Elekezi wa Kampuni ya Arges Afrika, Andrian Eradius, alisema ujenzi wa nyumba za Kwahani unakwenda vizuri na vifaa vyote vinapatikana kama kawaida ikiwamo mchanga na kuahidi kukamilika kama ilivyotarajiwa.

Alisema, wamefarajika kuona wanatembelewa mara kwa mara jambo ambalo linawapa ari ya kufanyaka kazi kwa bidii na kuahidi kazi hiyo kuikabidhi serikali ifikapo Septemba, mwaka huu.

Mradi wa nyumba za Kwahani ulianza rasmi ujenzi Oktoba 2, mwaka jana huku mradi wa ujenzi wa Mahakama Kuu ukianza mwishoni mwa mwezi huo na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, mwaka huu.



Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohamed Said, akizungumza na wafanyakazi wa wizara hiyo, jana, wakati wa utoaji wa elimu ya afya juu ya ugonjwa wa Corona. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wizara yatoa elimu wafanyakazi kujikinga corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amesema wizara yake imeamua kuwapatia elimu wafanyakazi wake ya kujikinga na virusi vya corona.

Alisema kutokana na kuenea kwa kasi kwa virusi hivyo duniani ipo haja ya kuwaelimisha watendaji wa wizara hiyo ili waweze kufanyakazi kwa umakini.

Akizungumza wakati wa utoaji wa elimu hiyo ya afya katika viwanja vya wizara hiyo Mazizini, mjini Unguja, Simai aliwataka wafanyakazi hao kuwa makini pamoja na kuifanyia kazi elimu waliyoipata na kuwa mabalozi wazuri wa kuwaelimisha wengine ili kujikinga na maradhi hayo.

Ofisa Mahusiano kutoka kitengo cha Elimu ya Afya, Ahmed Suleiman, alisema virusi vya ugonjwa wa corona husambaa haraka, hivyo ni vizuri kwa kila mmoja kuchukua tahadhari ili kuepuka maambukizo ya virusi hivyo.

Alisema Serikali ya Tanzania imetangaza rasmi kila raia atakaeingia nchini kutoka nchi iliyopata maambukizi, lazima awekwe kwenye maandalizi maalum kwa muda wa siku 14.

Kwa upande wao wafanyakazi wa wizara hiyo wameshukuru kwa hatua waliyochukua viongozi wao kwa kuwapa elimu watendaji wake, ambayo imewasaidia kujua kinga na athari za virusi vya korona.

# Abiria wa mabasi Songwe kunawa mikono mlangoni

**Na Manuel Kaminyoge,**
SONGWE

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemas Mwangela, amefanya ziara ya kushtukiza katika stendi ya mabasi ya Mlowo wilayani Mbozi na kutoa elimu juu ya njia za kujikinga dhidi ya virusi vya corona.

Kiongozi huyo wa mkoa aliagiza magari yote ya abiria yaweke maji ya kunawa mlangoni na akawataka madereva na makondakta kusimamia utekelezaji wa suala hilo kwa kuhakikisha abiria wote wananawa mikono kabla ya kuingia kwenye basi.

Alisema kwa kuzingatia utaratibu huo, itakuwa rahisi kujikinga dhidi ya janga hilo linaloitesa dunia kwa sasa.

Aliwataka wananchi kuachana na baadhi ya mila na desturi zikiwamo za kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana ambazo zinachagiza kuenea kwa kasi kwa virusi hivyo.

Alisema desturi hizo zinaonyesha kuwapo kwa upendo ndani ya jamii, lakini kwa hali ya sasa wananchi wanalazimika kuziacha kwa muda kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona.

"Ndugu zangu wananchi, msichukulie mzaha huu ugonjwa, ni hatari! Unaua na hauchagui dini wala kabila, chondechonde, naomba tuchukue tahadhari kwa kuhakikisha tunanawa mikono mara kwa mara kwa maji yanayotiririka, sitopenda kusikia mgonjwa wa corona kwa wananchi wangu wa Songwe," alisihi.

Neema Kalinga, miongoni mwa makondakta wa magari ya abiria mkoani humo, alisema agizo la mkuu wa mkoa litatekelezwa kwa kuwa ni muhinu kwa usalama wa afya zao na abiria.

Alisema tatizo kubwa ni uelewa wa wamiliki wa magari na kutokuwa na bajeti ya kumnunulia ndoo na dawa ya kunawia, hivyo akaiomba serikali kutoa elimu hata kwa wamiliki wa magari ili kuepusha mgogoro kati ya wamiliki na wafanyakazi wao.

"Tatizo linakuna bosi anapokosa uelewa, kuna mabosi wengine ndugu yangu ni shida, ukimwambia jambo, anahisi unataka kumwibia hela, kumbe ni agizo la serikali," alifafanua.

John Samson, abiria aliyekutwa na Nipashe katika stendi hiyo, alisema askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani wanapokagua mabasi, wasisahau kukagua uwapo wa maji ya kunawa mlangoni na vitakasa mikono.

Alisema kwa kufanya hivyo, itakuwa njia rahisi ya kuwafanya wenye magari kutekeleza agizo la mkuu wa mkoa.



Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemas Mwangela, akikagua mabasi na kutoa elimu ya njia za kujikinga na virusi vya ugonjwa wa corona kwa abiria, madereva na makondakta katika kituo cha mabasi cha Mlowo, wilayani Mbozi, mkoani humo, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake, vijana, wenye ulemavu wapewa mil. 118/-

**Na Sabato Kasika**

HALMASHAURI ya Wilaya Musoma, mkoani Mara, imetoa mkopo usio na riba wa Sh. milioni 118.4 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Akizungumza na gazeti hili, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Musoma, John Kayombo, alisema katika mkopo huo, kuna vikundi 16 vya wanawake ambavyo vimepata jumla ya Sh. milioni 98.

Mkurugenzi huyo alisema, kwa upande wa vijana ni vikundi viwili ambavyo vimepata Sh. milioni 11, wakati watu wenye ulemavu ni vikundi vitatu vilivyopata mkopo wa Sh. milioni 9.4

"Desemba mwaka jana, halmashauri yetu ilitoa mkopo usio na riba wa jumla ya Sh. 116.5 kwa vikundi 23, na sasa imetoa tena Sh. milioni 118.4 kwa vikundi 21," alisema Kayombo.

Mkurugenzi huyo alikitaja kikundi cha wanawake cha Upendo cha kijiji cha Chumwi, Kata ya Nyamrandirira kuwa ni miongoni mwa vikundi vilivyofaidika na mkopo huo kwa kukopeshwa Sh. milioni 7.5.

Kwa upande wake katibu wake msaidizi, Anna Stephen, alisema ni mara ya pili kupata mkopo wa halmashauri hiyo na kwamba mwaka jana walikopeshwa Sh. milioni tano.

"Kikundi chetu kina wanachama 19 na kinajishughulisha na kilimo cha mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula, kukodisha viti na kufuga kuku wa kienyeji, hivyo mkopo huu utasaidia kuimarisha shughuli zetu," alisema Anna.

Anna alifafanua kuwa kikundi chake kina mpango wa kuongeza ekari kutoka mbili hadi nne, kuongeza viti vya kukodi kutoka 20 vya sasa hadi kufikia 50 na pia kuboresha mabanda ya kufugia kuku.

Naye mwenyekiti wa kikundi cha walemavu cha Shivyawata cha kijiji cha Bwai Kumsoma, Kata ya Kiriba, Paskarina Magesa, alisema wao wamekopeshwa Sh. milioni tatu.

"Katika kikundi chetu tuliomba mkopo wa Sh. milioni saba, lakini tumepewa milioni tatu tu, hatuna jinsi inabidi tuzifanyie kazi kwa kuimarisha mradi wetu wa ufugaji wa kuku na kurejesha kwa wakati mkopo wetu," alisema Paskarina.

Alisema, hawawezi kupingana na uamuzi wa halmashauri, kwa vile ndivyo ilivyoamua, hivyo wanakubaliana nao ili kama kuna sehemu watakuwa wamekosea, basi warekebishe.

"Mwaka jana tulikopa Sh. milioni mbili na tukarejesha kwa wakati, na tulitarajia kuwa tungefikiwa na kupewa kile tulichoomba, lakini haikuwa hivyo, inabidi tukubaliane na hali," alisema.

# Simiyu wasuasua kwenda vituo afya

**Na Happy Severine,**
SIMIYU

IMEELEZWA kuwa wakazi wa mkoa wa Simiyu hawana uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa kuhudhuria katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Vituo hivyo vya huduma ni zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) mkoa wa Simiyu, Vedastus Joseph, wakati akitoa elimu kwa waandishi wa habari namna ya kujiunga na huduma zitolewazo na mfuko huo.

Alisema zoezi la usajili wa waandishi wa habari unafanyika kwa gharama ya Sh. 100,000 utaanza rasmi Aprili Mosi, 2020 hadi Juni Mosi, huku akiongeza kuwa ifikapo Julai Mosi zoezi hilo litakamilika na kwamba kadi kuanza kutoka kwa ajili ya kutumika.

Aliongeza kuwa mkoa wa Simiyu una jumla ya zahanati, vituo vya afya na hospitali 263 zinazotoa huduma za bima ya afya, hivyo wanatakiwa kuvitumia ipasavyo.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Chama cha Waandishi wa Habari mkoa wa Simiyu, Frank Kasamwa, alisema ni vema waandishi wakachangamkia fursa ya kujiunga na bima ya afya kwani ugonjwa aubishi hodi.

Paul Phaustine, mratibu wa chama cha waandishi wa habari mkoa wa Simiyu na Costantine Mathias, mwandishi wa gazeti la Uhuru na Mzalendo mkoa wa Simiyu, walisema kuwa wanashukuru kwa kupewa elimu hiyo ambayo imewapa mwanga.

"Naamini kwa sasa tutaweza kujiunga na bima ili tuweze kupata huduma za uhakika za matibabu kwa bei nafuu," alisema.

# Mji wa Kinshasa wafungwa kisa corona

**KINSHASA, Congo**

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imetangaza hali ya dharura na kuufunga mji mkuu wa Kinshasa au kujitenga katika hatua ya kupambana dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Rais wa DRC, Félix Tshisekedi alitangaza kuchukua hatua hizo juzi jioni kupitia Televisheni ya Taifa.

Rais Tshisekedi alisema kuwa pamoja na kufunga mipaka ya nchi, kusitisha safari za ndani na nje ya mji mkuu zikiwamo za mabasi, ndege na maji, utekelezaji wa haraka unahitajika.

Wiki iliyopita Jamhuri ya Afrika ya Kati ilitoa amri kwa raia wake kutokuwa na mizunguko.

Mpaka sasa DRC imeripotiwa kuwa na wagonjwa 48 wa ugonjwa wa virusi vya corona na watu watatu wamefariki kutokana na maambukizi ya ugonjwa huo.

Mji wa pili kwa ukubwa katika taifa hilo, Lubumbashi ulifungwa kwa saa 48, Jumatatu baada ya watu wawili kukutwa na maambukizi ya ugonjwa huo.

Wagonjwa hao mmoja alikuwa ni mwanamume mwenye miaka 47 na mtoto wake wa kiume wa miaka 13, walikuwa wametokea mji mkuu wa Kinshasa Jumapili.

Na siku hiyohiyo, kifo cha pili kilichotokana na ugonjwa wa corona kilitangazwa na Waziri wa Afya, Eteni Longondo huku wengine 30 walikutwa na maambukizi ya ugonjwa huo tangu MachI 10, mwaka huu.

Gavana wa Lubumbashi alitangaza saa 48 kwa mji wa Lubumbashi kufungwa, kuanzia Jumatatu wakati wakijaribu kubaini abiria 75 ambao wanapaswa kutengwa.

Kutokana na maambukizi hayo wabunge walimshauri Rais Tshisekedi kufunga miji ambayo ina maambukizi zaidi ya virusi vya corona ambayo ni Kinshasa na Lubumbashi.

Baadhi ya maamuzi ambayo Rais Tshisekedi aliyatanga ni pamoja na teksi kutobeba abiria zaidi ya watatu ingawa hapo awali walikuwa wanaruhusu watu zaidi.

**BBC**

# Mwanamfalme Uingereza apata maambukizi ya virusi vya corona

**LONDON, Uingereza**

MAAMBUKIZI ya ugonjwa wa virusi vya corona yameendelea kushika kasi duniani na sasa yamebisha hodi katika familia ya kifalme nchini Uingereza, kwamba mwanamfalme Charles amekutwa na maambukizi.

Taarifa iliyotolewa jana na msemaji wa familia hiyo, ilieleza kuwa mwanamfalme huyo wa Wales mwenye umri wa miaka 71, alionesha dalili ndogo za kuugua ugonjwa wa virusi vya corona jana, lakini bado amebakia kuwa katika afya nzuri," amesema msemaji.

Hata hivyo katika hali ya kushangaza, mke wake mwenye umri wa miaka 72 alipofanyiwa vipimo hakukutwa na maambukizi ya ugonjwa huo.

Taarifa kutoka makao yao ya Ufalme Clarence House ilieleza kuwa Charles na Camilla kwa sasa wamejitenga binafsi katika makazi ya Balmoral, na kuongeza kuwa mwanamfalme alikuwa akifanya kazi zake nyumbani kwa kipindi chote tangu tahadhari ilipotolewa ya ugonjwa huo.

Taarifa rasmi ilieleza kuwa: "Kulingana na ushauri wa serikali na wa kimatibabu, mwanamfalme na mkewe kwa sasa wamejitenga katika makazi huko Scotland".

"Vipimo vilichukuliwa na mamlaka ya kitaifa ya huduma za afya nchini Uingereza (NHS) eneo la Aberdeenshire, ambako walitimiza vigezo vya kupimwa".

"Huenda isiwe rahisi kutambua mwanamfalme aliambukizwa na nani virusi, ikizingatiwa idadi kubwa ya watu ambao aliokutana nao katika kazi zake za umma katika wiki za hivi karibuni".

**BBC**




Polisi nchini Hispania wakimwondoa bibi mtaani baada ya serikali kupiga marufuku watu kutoka nje. **Picha REUTERS**

# Wahamiaji 60 wakutwa wamefariki ndani ya lori

**MAPUTO, Msumbiji**

WATU wapatao 60 ambao wanaaminika ni wahamiaji haramu kutoka Ethiopia, wamekutwa wamekufa katika lori la mizigo nchini Msumbiji wiki hii.

Taarifa kutoka Jeshi la Polisi Msumbiji zinaeleza kuwa maofisa wake walisikia makelele ndani ya kontena lililokuwa limebebwa na lori hilo katika kituo cha ukaguzi kaskazini magharibi ya Jimbo la Tete, ambapo lori hilo lilisimamishwa baada ya kuvuka mpaka kutoka Malawi.

Maofisa wa usalama waligundua wahamiaji haramu walionusurika wapatao 14 pamoja na miili ya wahamiaji wengine walipofungua mlango wa kontena hilo. Wahamiaji hao wanaaminika kuwa walikufa kutokana na ukosefu wa hewa.

Walionusurika walichukuliwa kupatiwa matibabu katika hospitali ya eneo hilo. Dereva wa lori na mtu mwingine walikamatwa na kuwekwa mahabusi.

Msumbiji ambayo iko kusini mashariki mwa Afrika ni kituo cha kupitia wakimbizi wakijaribu kuingia Afrika Kusini, moja ya nchi katika bara la Afrika yenye viwanda vingi.

**VOA**

# Wananchi bilioni 1.3 wazuiwa kutoka nyumbani

**NEWDELH, India**

INDIA ambalo ndilo taifa kubwa duniani lenye idadi kubwa ya watu limeanza kutekeleza hatua ya kuwazuia majumbani wananchi wake wapatao bilioni 1.3 katika jitihada za kuzuia kuelea kwa ugonjwa wa virusi vya corona.

Hatua hiyo ya India isiyokuwa ya kawaida inalenga kuzuia kusambaa virusi hivyo na kuuelemea mfumo wake dhaifu wa huduma za afya kama vilivyofanya katika maeneo ya Ulaya, ambako idadi ya maambukizi inaendelea kuongezeka.

Wakati huohuo, nchini Marekani wabunge pamoja na ofisi ya Rais wameidhinisha mpango wa kutolewa msaada wa ndani wa Dola za Marekani trilioni 2, ili kuwasaidia walioathirika na virusi vya corona.

Nako nchini Italia ambako kumekuwa na matukio mengi ya vifo vitokanavyo na ugonjwa wa virusi vya corona matumaini yameanza kuonekana baada ya jana kuanza kupungua huku matukio ya maambukizi yakiongezeka.

Nchini Hispania, taarifa zinaeleza kuwa miili ya watu waliofariki imezidi kuongezeka hali iliyoilazimu serikali kutengeneza barafu ya zaidi ya kuihifadhi miili.

Jimbo la Hubei nchini China ambalo lilikuwa kitovu cha virusi hivyo, limeanza kuondoa jana vizuizi vya usafiri na hali ya kawaida imeanza kurejea.

**DW**

# Madereva waonywa mlipuko wa corona

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

MADEREVA wa magari madogo ya abiria yanayofanya safari za kutoka makao makuu ya Mkoa wa Kagera kwenda wilaya mbalimbali za mkoa huo, wametakiwa kuzingatia maelekezo ya abiria kutobanana katika magari, ili kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (Latra) Mkoa wa Kagera, Shedrack Malale, aliiambia Nipashe jana kuwa wamekwishatoa maelekezo kwa madereva wote, hivyo watakaobainika kukiuka maelekezo hayo, watachukuliwa hatua.

"Kutokana na elimu inayotolewa na ukaguzi unaofanyika, hatutegemei kukamata gari lolote likiwa limesimamisha abiria au limepakia abiria wamebanana, nafahamu wapo baadhi ya madereva wanakiuka, lakini wafahamu mkono wa sheria ni mrefu watakamatwa," alionya.

Alisema wanafahamu baadhi ya maeneo yana magari machache, lakini hiyo si sababu ya kupakia abiria kupita kiasi na wanachokifanya sasa, ni kutoa elimu kwa wasafirishaji na abiria wanaotumia magari hayo ili wawe mabalozi wa kufikisha ujumbe huo kwa wengine.

"Abiria wasiruhusu mtoa huduma aendelee kujaza abiria katika gari na endapo hatakubali kusikiliza ushauri wao, basi watoe taarifa katika mamlaka zinazohusika, lakini pia madereva na wasaidizi wao wajitahidi kuheshimu maelekezo yaliyopo kwa sababu wasipoyafuata, nao wanahatarisha maisha yao na familia zao," alionya.

Baadhi ya madereva waliozungumza na Nipashe akiwamo Pascrates John, anayeendesha gari la kutoka Manispaa ya Bukoba kwenda Mutukula mpakani wa Tanzania na Uganda, walisema wanajitahidi kuzingatia maelekezo ya kutopakia abiria wakiwa wamebanana, na kuomba serikali kuwachukulia hatua kali watakaobainika kukiuka.

"Kama sisi tunaoendesha magari yanayokwenda mpakani, tunajitahidi kuzingatia maana huko hatuwezi kujua abiria tuliowapakia wametokea wapi na kama wana maambukizo ya corona au hawana," alisema.

Dereva huyo aliiomba serikali kuendelea kutoa elimu kwa wananchi namna ya kujikinga na ugonjwa huo na kuhakikisha kunakuwa na maeneo ya kutosha ya kunawia mikono katika kituo kikuu cha mabasi cha Bukoba.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Bukoba, Dk. Hamza Mugula, alisema wamekwishatembelea maeneo mengi hasa yenye mkusanyiko mkubwa ikiwamo kituo kikuu cha mabasi na sokoni ili kusisitiza umuhimu wa kunawa mikono.

"Kunawa ndiyo kinga ya muhimu zaidi na tukinawa mikono tunapunguza maambukizo kwa asilimia kubwa, sabuni inayopaswa kutumika ni ya maji, lakini kama mwananchi hakuweza kupata sabuni ya maji basi atumie ya kawaida ya kipande," alisema.

Aliwasisitiza wananchi kuendelea kuzingatia maelekezo wanayopewa na wataalamu, na kuwa watakaobainika kukiuka kwa makusudi, uongozi wa manispaa hiyo kwa kushirikiana na vyombo vya dola watawawajibisha ili kuepusha kutokea athari zinazotokana na uzembe wa wananchi.




Mteja wa Shirika la Ndege la Precision Air, jijini Mwanza, akinawa mikono ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, kabla ya kuingia katika ofisi za shirika hilo, jana. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

## Jela miaka 30 kwa kubaka mwanafunzi

**Na Daniel Limbe,Chato.**

MKAZI wa Kata Katoro wilayani Geita, John Joseph, amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 jela baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka mwanafunzi wa kidato cha kwanza.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Chato, Denice Mrashani, baada ya kukamilika kwa ushahidi.

Hakimu Mrashani alisema kuwa licha ya utetezi uliotolewa na mshtakiwa, na uliowasilishwa na upande wa Jamhuri, Mahakama hiyo imejiridhisha pasipo kuacha shaka kuwa mshtakiwa ana hatia ya kumbaka mwanafunzi huyo ambaye (jina tunalihifadhi).

Awali Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Anosisye Erasto akishirikiana na Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Clemence Mango, walidai kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Februali 23, mwaka huu katika Kijiji cha Buseresere wilayani Chato mkoani Geita.

Walidai kuwa mshtakiwa akiwa na nia ovu alimrubuni (muathitika) kuwa anaitwa na dada mmoja (jina halikutajwa) kuwa anamsubiri kwenye eneo ambalo ni njia ya watembea kwa miguu wakati huku eneo hilo limezungukwa na vichaka.

Walidai zaidi kuwa baada ya kuitikia wito huo, ghafla alikabwa kwa nguvu na mshtakiwa kabla ya kuanza kumbaka.

Ilidaiwa kitendo hicho ni kinyume cha kifungu cha 130(1) (2) (a) pamoja na 131(1) cha Sheria ya Makosa ya Jinai kilichofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Hata hivyo, kabla ya kutolewa adhabu hiyo, mshtakiwa alipewa fursa ya kuiomba mahakama kumpunguzia adhabu,licha yamshitakiwa kudai kuwa hana utetezi wowote.

Kwenda jela kutumukia kifungo cha miaka 30 ili liwe fundisho kwa wengine wanaofanya vitendo vya kikatili.

# Ajira zingine 390 afya zatangazwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA MJINI**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Ummy Mwalimu, ametangaza ajira zingine 390 za madaktari kwenye hospitali za mikoa na rufani nchini, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Rais John Magufuli ya ajira 1,000 za madaktari.

Sambamba na hilo, amesema serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Benjamin Mkapa, imekamilisha taratibu za ajira kwa wataalamu wa afya 307 ili kuongeza nguvu ya kukabiliana na magonjwa mbalimbali vikiwamo virusi vya corona.

Waziri huyo aliwaambia waandishi wa habari jijini hapa jana wametoa nafasi kwa wenye sifa kuomba kwenye mikoa mitatu wanayopenda kufanya kazi, lakini kwa watakaochagua mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha wasitarajie kupangiwa kwenye mikoa hiyo.

"Hizi ni ajira 1,000 ambazo kati ya hizo 610 zitaenda Tamisemi na zingine 309 ni kwa hospitali za mikoa, madaktari 40 wataenda Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Benjamin Mpaka 20, Taasisi ya Mifupa Muhimbili 10, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete saba na Taasisi ya Saratani Ocean Road saba," alifafanua.

Alisema ajira hizo pia zitazingatia mikoa tisa ambayo ina uhaba mkubwa, mzigo wa magonjwa na upatikanaji wa huduma za afya na waombaji watatumia njia ya mtandao kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya," alisema.

Waziri huyo alisema Taasisi ya Benjamin Mkapa kupitia Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Ukimwi, imeajiri watumishi 307 ambao wanatakiwa kuripoti kwenye vituo vyao vya kazi ifikapo Machi 27 mwaka huu, yaani kesho.

"Wanaenda kuimarisha utoaji huduma na miongoni mwao, wapo wataalamu wa maabara ambao tunafikiria siku zijazo tutashusha huduma za kufanya vipimo vya awali vya corona," alisema.

Alisema wizara hiyo kwa kushirikiana na taasisi hiyo, iko katika hatua za mwisho kukamilisha ajira za wataalamu wengine 80 ambao watapangwa kwenye hospitali za rufani za mikoa 10 na hawatakiwa madaktari bali ni kada nyingine za afya.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA /MASHAMBA

**VIWANJA VINAUZWA,** Headline block ya viwanja vine inauzwa, Viko mbweni mpiji karibu na Shule ya Sekondari Mpiji . Eneo zaidi ya heka moja ) 4220 Sq mt . Viwanja Surveyed. Simu: 0711 506758 0787 445506, 0679 041220

## ELIMU/ MASOMO

**REGISTRATION OPPORTUNITIES**

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** located at salasala announces registration opportunities for Nursery and Primary School students. Call: 0713 327613.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA PASIPOTI



**ELIZABETH STANSLAUS MASUNGA**
anatangaza kupotelewa na passport, iliyo tolewa na Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Idara ya Uhamiaji Mwaka 2019 na inaisha muda wake mwaka 2029 yenye namba TAE 243983,

Kwa yeyote atakae iona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kwa kumb: **MZN/RB/530931/2020.**

115679902

## KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA

**HAMADI MOHAMED SHABAN** Anatangaza kupotelewa na hati ya nyumba yenye namba 186224/41.

Yeyote atakae iona hati hiyo ya nyumba anaombwa atoe taarifa ktk kituo chochote cha polisi taarifa ya polisi; **DSM/PHQ/RB/233455/2020.**

156807

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo:
MJINI-MOROGORO

**Usimamizi wa mirathi No;85/2020**

Ombi la SALMA J.NDOMBA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu JARIBUNI ISMAIL NDOMA. Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/04/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 24/03/2020.




115679802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMED NAZEER PARAPURAM** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 409 DPP MAZDA.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/SEL/RB/41055/2020.

156809

## KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA

**HAMADI MOHAMED SHABAN** Anatangaza kupotelewa na hati ya nyumba yenye namba **186224/41.**
Yeyote atakae iona hati hiyo ya nyumba anaombwa atoe taarifa ktk kituo chochote cha polisi taarifa ya polisi; **DSM/PHQ/RB/233455/2020.**

11568022

## KUPOTEA KWA KADI

**Richard Emmanuel Maduhu** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T. 774 BZZ aina ya TOYOTA IPSAM, yenye Engine namba 357146410 Chassis namba SXM107110345.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake.

Taarifa ya Polisi.: **KAH/TR/RB/119/2020**

115680302

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA OFFA YA KIWANJA

KHAMISI MOHAMED MALUNDI MKAZI WA MTAA WA KAUNDA MANISPAA YA SHINYANGA

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFFA YA KIWANJA NAMBA 31 KITALU 'G' MJINI KATI MANISPAA YA SHINYANGA, AMBAYO ILIPOTEA MWAKA 2019 MAENEO YA SHINYANGA. KWA YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA KHAMIS MOHAMED MALUNDI KWA SIMU NAMBA 0677186853

**RB NAMBA SHY/RB/ 2020, CONTOL NAMBA 9910812112044.**

115680102

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA
KIGOMA
MAHALI: KIGOMA
MAOMBI NA 56 MWAKA 2017
HAMIS NKULUZI............MWOMBAJI
DHIDI YA
KIMBEMBE AUCTION MART LTD AND TRIBUNAL BROKERS..................WAJIBU MAOMBI

**WITO WA KUITWA SHAURINI**

KWA: KIMBEMBE AUCTION MART LTD AND TRIBUNAL BROKERS

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kusikilizwa tarehe 30 mwezi 3 mwaka 2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mhe. F.Chinuku Mwenyekiti wa Baraza .Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 14 mwezi wa 2 mwaka 2020.



1156880002


Uza,
Chenye
Thamani Kubwa Kwa
Kutangaza Nasi
Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII



OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# SOLSKJAER

## AMWINDA OSIMHEN WA LILLE

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amemtaja mshambuliaji wa Lille, Victor Osimhen kama 'kipaumbele' chake kwenye usajili wa kipindi cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa gazeti la Le10 Sport, Manchester United ipo tayari kupambana na Real Madrid kwenye mbio za kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21.

Osimhen ameonesha kiwango cha kuvutia pale Lille msimu huu, akifunga mabao 17 katika mechi 35 za Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Kwa mujibu wa ripoti ya gazeti hilo, Solskjaer anamtaka mshambuliaji huyo ili kuiongezea nguvu safu yake baada ya juzi kuripotiwa kuwa Odion Ighalo anatarajiwa kusajiliwa rasmi hapo Old Trafford.

Gazeti la Daily Mail lilibainisha kwamba, Man United wanajiandaa kumsajili Ighalo kwa mkataba wa kudumu kipindi cha majira ya joto kwa pauni milioni 15.

Ighalo alijiunga na Man United kwa mkopo Januari akitokea klabu ya Shanghai Shenhua ya nchini China.

## CHELSEA YAMRUHUSU WILLIAN KUMFUATA MKEWE BRAZIL

**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea imeripotiwa ipo tayari kumwachia Willian kurudi nyumbani kwao Brazil kuungana na familia yake baada ya winga huyo kuachwa mpweke jijini London kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Baada ya serikali ya Uingereza kuzuia watu kutosafiri na kufutwa kwa safari za ndege, Willian alijikuta amebaki peke yake jijini London huku mke na watoto wake wakiwa nchini Brazil na sasa klabu inampa ruhusa ya kwenda kuungana nao.

Kwa mujibu wa gazeti la Sun, Willian atapewa ruhusa hivyo licha ya wachezaji wengine wa Chelsea na wananchi wa Uingereza kuamuliwa kutotoka nje ya nyumba zao kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Mke wake, Vanessa Martins na mabinti zake wawili, Valentina na Manuella wapo nyumbani kwako nchini Brazil.

Ligi Kuu ya England imesimama hadi Aprili 30 na sasa Willian akifika Brazil atabakia huko hadi ligi itakapoanza tena.

Willian hivi karibuni alinukuliwa na televisheni ya Globo Spor akisema: "Kwa wakati huu nipo peke yangu. Mke wangu na mabinti zangu wapo Brazil.

"Niliweka ratiba wao watangulie kwanza, na mimi nilitarajiwa kujiunga nao haraka. Lakini sasa hadi niruhusiwe kwanza."

# Bayern yamwania kipa wa Barcelona

**MUNICH, Ujerumani**

KLABU ya Bayern Munich imeripotiwa kuwania saini ya golikipa wa Barcelona, Marc-Andre ter Stegen's.

Kwa mujibu wa gazeti la Bild, Bayern inataka kumsajili kipa huyo kwa sababu ya majeruhi ya mara kwa mara yanayomkumba golikipa namba moja wa timu hiyo, Emanuel Neuer.

Ter Stegen's mapema mwezi huu alikataa kuongeza mkataba huku akishinikiza anahitaji mkataba mnono zaidi utakaomfanya mchezaji wa pili kulipwa mpunga mrefu nyuma ya Lionel Messi.

Kwa sasa kipa huyo ana umri wa miaka 27, ambapo anaonekana kijana zaidi ya Neuer ambaye ana miaka 33, hivyo Bayern wanawekeza nguvu zaidi wakiamini watamtumia kwa muda mrefu zaidi.

Taarifa kutoka Ujerumani zinasema kumekuwa na mkwaruzano kati ya Neuer na Rais wa klabu ya Bayern, Franz Beckenbauer, jambo ambalo linaonyesha kuna asilimia kubwa ya Ter Stegen kuingia klabuni hapo msimu ujao. Mpaka sasa Barcelona hawaaonekani kuwa na nia ya kumpa mkataba mpya.



# MESSI, GUARDIOLA
## WATOA SH. BILIONI 4.8 KWA CORONA

**BARCELONA, Hispania**

HOSPITALI ya Barcelona imemshukuru, Lionel Messi kwa kutoa msaada wa fedha ili kukabiliana na janga la mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19) .

Nahodha huyo wa Barcelona ameungana na Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola kwa kila mmoja kutoa euro milioni moja sawa na Sh. bilioni 2.4 za Tanzania kwa ajili ya kusaidia kukabiliana na janga la virusi hivyo vya corona ambapo zaidi ya watu 40,000 wamethibitishwa kuambukizwa nchini Hispania.

Ligi mbalimbali za soka pamoja na matukio ya kimichezo duniani yamesimamishwa duniani kote kwa ajili ya kukabiliana na mlipuko huo.

Messi ameungana na Guardiola kutoa msaada jijini Barcelona ambao kila mmoja ametoa euro milioni moja, hivyo jumla kwa wote wawili kiasi walichokitoa kwa fedha za Tanzania ni sawa na Sh. bilioni 4.8.

Messi mshindi mara sita wa Ballon d'Or - ametoa mchango katika hospitali ya Barcelona.

Twitter kutoka hospitali hiyo iliandika: "Leo Messi ametoa mchango wa kupambana na COVID-19 hospitalini kwetu.

"Asante sana Leo, kwa mchango wako na kujitolea."

# Kane akaribia kurudi dimbani

**LONDON, England**

HARRY Kane amebainisha "kuendelea vizuri" na anaweza kurudi kwenye mazoezi na wachezaji wenzake wa Tottenham "ndani ya wiki mbili au tatu" zijazo.

Nahodha huyo wa timu ya taifa ya England na Spurs, amekuwa nje ya dimba tangu alipoumia misuli wakati wa mchezo wa kipigo wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Southampton siku ya mwaka mpya.

Kane ameonyesha maendeleo mazuri na anaweza kurudi kwenye mazoezi kamili mwezi ujao na ameiambia televisheni ya Spurs: "Siko mbali sana, natarajia kurudi kwenye mazoezi na timu ndani ya wiki mbili au tatu zijazo.

"Nipo kwenye hali nzuri, najisikia kuwa fiti, sasa ninachofanya ni kujenga ufiti wangu.

"Kwa sasa najituma kwa bidii, huku nikiendelea kupona taratibu na naamini ndani ya mwezi nitakuwa fiti kabisa."

Msimu wa Ligi Kuu ya England umesimama kwa muda hadi Aprili 30 kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Kabla ya kuumia Kane alifunga mabao 11 katika mechi 20 za Ligi Kuu msimu huu.



# Mourinho mkali lakini anapendwa - Ballack

**LONDON, England**

JOSE Mourinho "ni mkali sana" kama kocha, lakini wchezaji wake wengi wanapenda kuzungumza nae kwa upendo, kwa mujibu wa Michael Ballack.

Ballack alisajiliwa na Mourinho pale Chelsea mwaka 2006 na alifanya kazi chini ya kocha huyo wa sasa wa Tottenham hadi alipomaliza kipindi chake cha kwanza pale Stamford Bridge mwaka uliofuata.

Staili yake ya ukali ya kocha huyo raia wa Ureno imesababisha kukwaruzana na wachezaji hasa wenye majina makubwa katika klabu alizoziona kuanzia Real Madrid, Manchester United na Inter Milan.

Lakini Ballack anahisi Mourinho ana ubora wa kuvutia kama kocha licha ya ukali wake kwa wachezaji.

"Kwa uhakika utavutiwa na mbinu zake na hamasa yake," amesema Ballack akinukuliwa na Sky Sports.

"Kufanya kazi na kocha kama yeye kilikuwa kipya kwa upande wangu. Alinivutia na kwa hakika nijisikia amani sana hasa kwa maamuzi yangu ya kusajiliwa Chelsea.

"Mahusiano yetu bado yako vizuri na yeye. Huwezi kukuta wachezaji wengi wakimzungumzia vibaya yeye."

Kuhusu Mourinho kuondoka ghafla Chelsea Septemba 2007, Ballack aliongeza: "Nilipata uzoefu wa kutosha kumwelewa."

"Usiposhinda kitu, kocha ndio mtu anayekuwa dhaifu zaidi kwenye timu na anaweza kufukuzwa wakati wowote.

"Alikuwa kwenye mwaka wake. Ukiangalia wastani wa muda wa kocha muda aliofanya kazi kwenye klabu, kwa hakika ulikuwa ni muda mzuri."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MANE ATAENDA MADRID, SALAH ATASEPA - SISSOKO

Liverpool ni wazuri sana na watajua namna ya kuziba nafasi yake kama ataondoka...

**LIVERPOOL, England**

SADIO Mane ataitema Liverpool ili kujiunga na Real Madrid, kwa mujibu wa kiungo wa zamani wa miamba hiyo ya Anfield, Momo Sissoko, wakati wa kuondoka kwa Mohamed Salah kunaweza kuwa vizuri kwa 'Wekundu' hao.

Kiungo huyo wa zamani wa Liverpool, Sissoko anaona Real itahitimisha mchakato huo kwa kumpata mshambuliaji mmoja kati ya hao wawili inaowawinda na yeye anaamini kuna uwezekano zaidi kwa Mane kutua Real Madrid kuliko Salah.

Salah na Mane, wote ni miongoni mwa wachezaji wenye thamani zaidi duniani na wamekuwa katika rada za Zinedine Zidane tangu majira ya joto yaliyopita na wanaweza kuondoka kama watatwaa kwa mara ya kwanza ubingwa wa Ligi Kuu England.

Tayari wamefanikiwa kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka jana, mastaa hao watakuwa na vitu vidogo watakavyohitaji kushinda tena wakiwa na Liverpool kama wakitwaa ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu.

Wekundu hao wapo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England kwa pointi 25 zaidi wakati huu wakiwa wamebakiza mechi tisa za kucheza kabla ya msimu kumalizika na wakihitaji kushinda michezo miwili tu ili kutwaa ubingwa huo.

Lakini hiyo inaweza kumaanisha Salah na Mane - haswa wanaweza kuwa wa mwisho kama watajiunga na Real Madrid majira haya ya joto.

Sissoko aliliambia EuropaCalcio: "Ninamwona Mane akiwa Real Madrid [kuliko Salah].

"Yeye [Mane] ana tabia ambazo Zidane anazitaka... Nadhani Mane atakwenda Real Madrid.

"Sijui kama Salah ataendelea kuwapo Liverpool. Lakini kama ataondoka, kuondoka kwake kutakuwa kuzuri kwa timu.

"Liverpool ni wazuri sana na watajua namna ya kuziba nafasi yake."

## KWA UFUPI

**STERLING ROHO IPO LIVER**

MSHAMBULIAJI wa Manchester City na England, Raheem Sterling, 25, bado ana mapenzi na Liverpool licha ya namna alivyoondoka na kujiunga na City. ***(Sky Sports)***

**ARSENAL, LIVER KWA THIAW**

Liverpool, Manchester City na Arsenal zinavutiwa na beki wa Schalke mwenye kimo cha futi sita na inchi tatu (6ft 3in), mzaliwa wa Mjerumani, Malick Thiaw, 18, ambaye anaruhusiwa kuuvunja mkataba wake kwa pauni milioni 6.9. ***(Mail)***

**CHELSEA SASA KWA TAGLIAFICO**

CHELSEA inavutiwa na beki wa Ajax, Muargentina Nicolas Tagliafico, 27, baada ya kuachana na mpango wao wa kumsajili beki wa pembeni wa Leicester, Ben Chilwell. ***(Calciomercato via Daily Express)***

**POGBA AITIA SHAKA UTD**

Manchester United bado inaendelea kujiamini kwamba mshindi wa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa, kiungo Paul Pogba, 27, atabaki Old Trafford na hofu kama klabu kubwa za Ulaya zitamudu kumnunua. ***(ESPN)***

**MADRID NAYO KWA HAALAND**

Real Madrid inataka kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Mnorway Erling Braut Haaland, 19, majira ya joto yajayo ingawa Manchester United na Tottenham pia zinavutiwa naye. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

**FABREGAS: KISA KUSEPA ARSENAL**

Cesc Fabregas amesema aliondoka Arsenal na kujiunga na Barcelona mwaka 2011 kutokana na sababu kibao, ikiwa ni pamoja na uhusiano wake na baadhi ya wachezaji wenzake wa zamani hapo Camp Nou, presha ya kushinda makombe na kutokana na klabu kushindwa kufanya usajili mzuri. ***(skysports)***

**INTER, LAZIO ZAMTAKA GIROUD**

Inter Milan na Lazio zinajiandaa kuingia vitani kuisaka saini ya mshambuliaji wa Chelsea, Mfaransa Olivier Giroud, ambaye ana mabao matatu katika mechi 13 alizocheza msimu huu. ***(Tuttosport)***

**JUVE WAACHIWA, DYBALA BADO**

KARANTINI ya wachezaji wa Juventus pamoja na viongozi ilitarajiwa kumalizika jana, Jumatano na wachezaji kuruhusiswa kurejea nyumbani kwao. Hata hivyo, wachezaji Daniele Rugani, Blaise Matuidi na Paolo Dybala wataendelea kubaki, wakati wakiendelea kutibiwa maambukizi ya virusi vya corona. ***(Gazzetta dello Sport)***

**CHELSEA KUMFUATA CUCURELLA**

Chelsea ipo tayari kumsajili beki wa pembeni wa Getafe, Mhispania Marc Cucurella, 21, majira haya ya joto kwa kwa pauni milioni 23. ***(Diario Sport - in Spanish)***

**SMALLING KUMPISHA KOULIBALY**

BEKI wa Manchester United, Chris Smalling, 30, ambaye anacheza kwa mkopo Roma, anaweza kujiunga na klabu hiyo jumla kama 'Mashetani Wekundu' hao watamsajili beki Msenegal Kalidou Koulibaly kutoka Napoli. ***(Gazzetta dello Sport via Football Italia)***

**PLEA ALIVYOKWAMISHWA BARCA**

Borussia Moenchengladbach ilikataa mpango wa Barcelona kumtaka mshambuliaji wao, Mfaransa Alassane Plea, 27, mwishoni mwa dirisha la usajili lililopita la Januari. ***(Sport Bild - in German)***

HABARI MICHEZO

# AZAM YAJIPANGA KUSAKA DAWA YA WASHAMBULIAJI

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC, umesema 'unaumiza kichwa' kutafuta mbinu ya kulimaza tatizo la 'ubutu' kwenye safu ya ushambuliaji wa timu hiyo ambayo ni mabingwa watetezi wa mashindano ya Kombe la FA.

Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat' ameliambia gazeti hili jijini Dar es Salaam jana kuwa tatizo la umaliziaji ndilo linaloimaliza timu yao kwa sasa licha ya kuwa katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Popat alisema washambuliaji wao wanapoteza nafasi nyingi za kufunga, hali inayowafanya kuwa na idadi ndogo ya mabao.

Alisema wamekuwa wakiutazama mwenendo wa timu na aina ya matokeo jambo linalowafanya watafute mbinu ya kulimaliza tatizo hilo pale msimu huu utakapomalizika.

"Kweli tuna tatizo kwenye safu ya ushambuliaji, hilo lipo wazi lakini kwa sasa hatuwezi kufanya jambo lolote kulimaliza, tulichokubaliana ni kuboresha mikataba kwanza ya wachezaji tulionao, halafu kuongeza nguvu kazi mpya.

"Katika dirisha la usajili tutaleta washambuliaji ambao watakuwa suluhisho la tatizo letu, na kufanikiwa kufikia malengo yetu kwa msimu ujao," alisema Popat.

Aliongeza kwa sasa wanasubiri mapendekezo rasmi kutoka katika benchi la ufundi la timu hiyo.

Ligi Kuu Bara ikiwa imesimama huku safu ya Azam FC ikiwa imefunga mabao 37 na Mzambia Obrey Chirwa akiongoza mwenye kupachika magoli kwa kufunga mabao nane.

TUNACHEZA...



Wachezaji wa timu ya tenisi ya wenye ulemavu wakifanya mazoezi katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# ZFF yakumbusha msisitizo corona

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limewataka wachezaji, viongozi, mashabiki na wadau wa mchezo huo visiwani humo kutoa kauli na machapisho mbalimbali juu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona (COVID 19).

Katibu Mkuu wa ZFF, Mohamed Ali Hilali, alisema jana ugonjwa huo ni janga la kimataifa na kamwe haupaswi kudharauliwa kama baadhi ya wananchi wanavyofanya.

Hilali alisema ZFF inaendelea kuungana na serikali kwa kuzifanyia kazi kauli na maagizo yote yanayotolewa na Waziri wa Afya wa Zanzibar, Hamad Rashid Mohamed katika kupambana na janga la hilo na corona .

Alisema ZFF inashangazwa kuona baadhi ya watu na taasisi bado zinaendelea kucheza mpira kwa namna ya kushindana (mechi za kirafiki na mashindano yasio rasmi) katika maeneo ya Unguja na Pemba mashambani wakiamini huko hakuna maambukizi.

"Ndugu wanasoka, niwaombe tutekeleze kwa vitendo maagizo na maelekezo tunayoyapata kutoka serikalini na kwa watu tuliowapa dhamana ya masuala ya afya, tusichukulie masihara na wala kuleta dharau katika suala hili... naomba tuendelee kufuata maagizo katika kipindi hiki ambacho dunia inahangaika na ugongwa wa corona," Hilali alisema.

# Kocha Ndanda alia corona kuwatibulia

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Ndanda FC ya mkoani Mtwara, Abdul Mingange, amesema uamuzi wa kusimamishwa kwa Ligi Kuu Bara umemweka katika 'presha ya juu' kwa sababu umewaondoa wachezaji wake katika kasi ambayo alikuwa ameitengeneza.

Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na ligi nyingine mbalimbali hapa nchini na duniani, zimesimama ili kupambana na maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19), ambavyo vinaisumbua dunia kwa sasa.

**Akizungumza na gazeti hili juzi, Mingange alisema uamuzi wa kusimamishwa ligi ulichukuliwa kwa mis ingi ya kina, lakini ana mashaka na vijana wake kurejea kwenye kasi ambayo walikuwa nayo kabla ya uamuzi huo kutolewa.**

Mingange alisema licha ya kuwapa wachezaji wake maagizo ya kufanya katika muda huo wa mapumziko, hana imani watakaporejea kama watakuwa kwenye ubora wa kuhimili ushindani wa ligi hiyo iliyoko katika hatua ya lala salama.

"Licha ya kuwapa mikakati ya kufanya wanapokuwa nyumbani, lakini bado nitahitajika kufanya kazi kubwa ya ziada ili kuhakikisha wanarejea katika kasi yao ya awali ili kupambana kupata matokeo katika michezo yetu yote," alisema Mingange.

Alisema anahitaji kutoka katika nafasi walipo katika msimamo wa ligi ili kujinasua kwenye janga la kushuka daraja.

Ndanda ipo nafasi ya 16 kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 31 zilizotokana na mechi 29.

# Coastal Union yapotezea kambi

**Na Shufaa Lyimo**

HUKU ikiwa na uhakika wa kutoshuka daraja, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, amesema kikosi chake hakitaingia kambini mapema kwa sababu ya kujiepusha na maambukizi ya virusi vya corona (COVID 19).

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda alisema wachezaji wake wataendelea kufanya mazoezi binafsi mpaka pale serikali itakapotangaza hali ya maambukizi imetengamaa.

"Sina haraka na kuingia kambini, ninaogopa sana ugonjwa ambao umeibuka sasa hivi, sifanyi mzaha, ni janga la taifa," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema kwa upande wake amesimamisha kazi zote za mpira mpaka hapo itakapotajwa tarehe mpya ya kurejea kwenye kazi za mikusanyiko.

"Kila mchezaji nimempa jukumu lake katika kipindi hiki kwa kutambua Ligi Kuu msimu huu ina ushindani, naamini watafanyia kazi yale maagizo niliyowapa," Mgunda alisema.

Aliongeza msimu huu ligi imekuwa na changamoto zaidi na kusema anahitaji kujipanga vizuri ili wafikie malengo waliyokiwekea wakati msimu unaanza.

"Mpaka sasa hali bado haijatengemaa, binafsi nimetulia na familia yangu nyumbani huku tukiwa tunajilinda na ugonjwa huo," alisema kocha huyo.

Kuhusu harakati za usajili alisema hatakurupuka kufanya mchakato huo, lakini anaamini ataongeza wachezaji wenye uwezo na uzoefu.

"Nitasajili wachezaji ambao naamini wataipa mafanikio timu yangu na sitasajili mchezaji kwa ukubwa wa jina," alisisitiza.

# Michezo

Alhamisi Machi 26, 2020

Nipashe




Mane ataenda Madrid, Salah atasepa - Sissoko

HABARI UK 30

**ANAITAKA...**




Kiungo wa Yanga, Papy Tshishimbi, anayeelezwa kuingia katika mawindo ya watani zao, Simba. **PICHA: MAKTABA**

# TSHISHIMBI AIITA SIMBA SC MEZANI

●●●GSM yajiweka kando Yanga, asema hata Azam ikifika dau anakwenda, huku....

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI nahodha wa Yanga, Papy Tshishimbi akiwaita mezani Simba, hali ndani ya klabu hiyo imekuwa 'tete' baada ya Kampuni ya GSM kutangaza rasmi itajiweka pembeni kufanya shughuli mbalimbali za uendeshaji ambazo haziko kwenye mkataba, imefahamika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Tshishimbi alikiri kufanya mazungumzo na Yanga na kupokea nakala ya mkataba mpya, lakini bado hajasaini kwa sababu klabu hiyo haijatimiza dau ambalo analitaka.

Tshishimbi alisema mpira ndio kazi yake na yuko tayari kujiunga na Simba, Azam au Namungo endapo watafikia dau lake analolitaka atasaini na kwenda kuitumikia.

"Mkataba wangu ulikuwa ni wa mwaka mmoja, unamalizika mwezi wa nane, nimebakiza miezi minne tu, wameshaniletea mkataba mpya, ila kuna mambo bado tunaongea, tunazungumza, wakiwa tayari tutamalizana, mimi sichagui," alisema Tshishimbi.

Aliongeza kuwa ana familia, hivyo anahitaji kusaini mkataba ambao utakuwa mnono kwake kwa sababu kila mmoja kwenye kazi yake anahitaji mafanikio.

Hata hivyo, taarifa kutoka ndani ya klabu ya Yanga zinaeleza kuwa Tshishimbi amegoma kusaini mkataba mpya baada ya kusikia mshambuliaji Bernard Morrison amepewa donge nono, lakini chanzo kikingine kilieleza kwamba tayari alishasaini mkataba wa awali wa kujiunga na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba.

Aidha, kuhusu tamko la GSM limetolewa siku chache baada ya kampuni hiyo kukamilisha mchakato wa kumwongezea mkataba mpya wa miaka miwili Morrison, ambaye alitajwa kuwindwa na watani zao, Simba.

Kwa mujibu wa barua ya GSM iliyopatikana jijini jana kwenda kwa uongozi wa Yanga ambayo iliandikwa juzi, Machi 24, mwaka huu na kusainiwa na mmoja wa wakurugenzi wa kampuni hiyo, Feisal Mohammed, inasema sasa haitafanya jambo lolote ambalo lipo nje ya mkataba.

Taarifa ya kampuni hiyo ilitaja shughuli ambazo ilizifanya kwa mapenzi ya kurejesha heshima ya klabu hiyo bila ya kuwapo kwenye mkataba kuwa ni pamoja na kumrudisha kikosini beki, Lamine Moro ambaye alikuwa ameondoka baada ya kutangaza kukatiza mkataba wake, kuwasajili Morisson, Ditram Nchimbi, Haruna Niyonzima na Adeyum Saleh kwa lengo la kukiongezea nguvu kikosi chao wakati wa dirisha dogo.

Wadhamini hao pia wameeleza kuwa walilipa gharama za kumleta Kocha Mkuu, Luc Eymael na wasaidizi wake, mishahara, usafiri wa ndani, nyumba na tiketi za kwenda na kurudi makwao za makocha hao huku pia wakilipa mishahara ya wachezaji na bonasi za ushindi katika mechi zote walizoshinda tangu Desemba mwaka jana.

Kampuni hiyo pia ilitoa ahadi ya Sh. milioni 200 endapo wataifunga Simba, ahadi ambayo imeshatekelezwa baada ya ushindi wao wa bao 1-0, wamelipia gharama za kambi, usafiri wa ndege wa timu kuelekea katika baadhi ya mechi na kugharamia uwanja wa mazoezi, ukarabati wa uwanja, ununuzi wa vifaa vya mazoezi na kulipa baadhi ya madeni ya nyuma ya usajili wa wachezaji.

"Haya yote yamefanyika kwa mapenzi mema kwa klabu yetu bila kujali gharama nyingi na kubwa tunazolipa, pia katika kuelekea mabadiliko ya kiundeshaji wa klabu, GSM ilitafuta wataalamu kuja kushauri na kusaidia mabadiliko ya kimfumo na kupata timu rafiki kubwa ya barani Ulaya (Benfica)," ilisema sehemu ya barua hiyo.

Iliongeza kuwa, wanasikitika kusikia baadhi ya viongozi wakisema kampuni hiyo inawaingilia viongozi na sasa itafanya shughuli ambazo ziko kwenye makubaliano tu.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alipoulizwa kuhusu barua hiyo ya GSM, alisema haijafika klabuni kwao na wao wanaamini wataendelea kushirikiana vema na kampuni hiyo kama ilivyokuwa awali.

Bumbuli alisema anaamini kila kitu kitakwenda vizuri na hakuna mwanachama yeyote wa klabu hiyo yuko tayari kuona mambo yanakwenda 'kombo'.

## Sven: Mapumziko corona safi Simba

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, amesema anajivunia mapumziko ya siku 30 kwa kudai itasaidia wachezaji wake watakaporejea kuwa fiti zaidi.

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni, Sven alisema wachezaji wake walikuwa wamechoka kutokana na kucheza mechi mfululizo jambo ambalo lilikuwa likimpa wakati mgumu kwenye kupanga kikosi na kulazimika kuwapa mapumziko wachezaji wake.

Alisema watatumia muda wa mapumziko kurejea kwenye ubora kutokana na kila mmoja amempa programu ya mazoezi binafsi.

**"Kwa sasa watapata muda wa kupumzika na kurejea kwenye ubora wao, ninaamini itakuwa bora kwetu na nafuu kwani itawafanya wachezaji kuwa makini kuufukuzia ubingwa ambao tunautaka kwa sasa," alisema Sven.**

Alisema alikuwa akitumia nguvu katika maandalizi yao na kuwapa mapumziko mafupi jambo ambalo lilikuwa likiwafanya wasiwe fiti kwa asilimia mia.

Simba ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 71 zilizotokana na mechi zao 28 walizocheza hadi ligi hiyo inasimama kuepuka kuenea maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19).



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >